**20 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Nane – Tarehe 20 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na usalama kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya, Mbunge wa Manyoni Mashariki, sasa aulize swali lake.

Na. 351

### Kurasimisha Mabalozi wa Nyumba Kumi

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kurasimisha viongozi wa nyumba kumi (mabalozi) kama sehemu ya kuimarisha usalama wa raia?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ulinzi na usalama katika ngazi ya msingi kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, usalama wa raia umeendelea kusimamiwa na vyombo vya usalama kwa kushirikiana na wananchi kupitia mfumo wa uongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika ngazi za msingi ikiwemo

Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa, Vitongoji na Mabalozi. Serikali itaendelea kuboresha mfumo wa utambuzi na usalama katika ngazi ya msingi kwa kupitia mfumo wa uongozi wa Serikali za Mitaa uliopo ili kuongeza ufanisi katika kuimarisha masuala ya usalama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa Serikali imekiri kwamba mabalozi nao ni sehemu muhimu ya kuimarisha ulinzi na usalama na maendeleo ya halmashauri zetu, sasa nini mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba wanatumia kada hii ya mabalozi kuwajengea uwezo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa mwaka jana ulikuwa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na tayari tulishapata Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanawajengea uwezo? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ni kweli kwamba, Viongozi wa Serikali za Mitaa wakiwemo Mabalozi, Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa ni nguzo muhimu katika usalama wa raia katika maeneo yao. Hata hivyo, jambo la msingi kwanza usalama unaanza kwa kila mwananchi mwenyewe kutimiza wajibu wake na kutoa taarifa pale anapoona kuna viashiria vya kuathirika kwa usalama katika eneo hilo na mabalozi ndiyo viongozi wa kwanza katika mitaa yetu ambao wanapokea taarifa hizo ambazo zinafanyiwa kazi kwa ngazi ya ubalozi, kijiji, mtaa na hatua zinazofuata ngazi ya kata mpaka wilaya, mpaka ngazi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imeendelea kuwajengea uwezo

Waheshimiwa Mabalozi na wanafanya kazi zao, lakini zoezi hili ni endelevu. Tutaendelea kuwajengea uwezo mara kwa mara ili wawe na ufanisi mkubwa zaidi katika kutambua viashiria vinavyoathiri usalama, lakini pia kuchukua hatua stahiki kwa wakati ili kuhakikisha kwamba jamii yetu inakuwa salama zaidi. Hivyo hivyo, viongozi ambao wamechaguliwa mwaka 2024, Wenyeviti wa Vijiji, Mitaa na Vitongoji wataendelea kujengewa uwezo huu ili kuwa na uwezo mzuri zaidi wa kusimamia masuala ya usalama, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 352

**Ujenzi wa Barabara wa Uchira – Kisomachi – Kolarie**

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Uchira - Kisomachi kwa kiwango cha lami katika Jimbo la Vunjo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianza kutekeleza ujenzi wa Barabara ya Uchira – Kisomachi - Kolarie kwa kiwango cha lami mwaka 2019/2020 ambapo kilometa 1.4 zilijengwa kwa shilingi milioni 694.575. Aidha, mwaka 2023/2024 shilingi milioni 724 zilitolewa kwa ajili ya kujenga kipande chenye urefu wa kilometa 0.8 ambapo kazi imefikia 40%. Katika mwaka 2024/2025 Serikali imeendelea na ujenzi wa tabaka la lami kwa urefu wa kilometa 0.8 kwa gharama ya shilingi milioni 474.56. Ujenzi unaoendelea sasa utakapokamilika utafanya jumla ya urefu wa kilometa 3.0 za lami kuwa zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika mwaka 2025/2026 Serikali imepanga kujenga kilometa moja kwa kiwango cha lami kwa shilingi milioni 500. Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja katika Jimbo la Vunjo kwa kujenga, kukarabati na matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuena Bushiri, swali la nyongeza.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, barabara hii ina kilometa 10.9. Barabara hii ni korofi sana kipindi cha mvua, mnamo mwaka 2019 wananchi walijenga kilometa 1.4 kwa nguvu zao na Serikali ikaahidi kwamba itamalizia kilometa zilizobakia. Wananchi wa Vunjo wanataka kujua, je, ni lini Serikali itakamilisha hizo kilometa zilizobakia? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha inaendelea kuimarisha mtandao wa barabara zetu hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA* na ndiyo maana utaona katika kipindi cha Awamu ya Sita bajeti ya *TARURA* imeongezeka maradufu. Bajeti ya *TARURA* ilikuwa ni shilingi bilioni 275 kwa mwaka, lakini tunavyozungumza wakati huu tunatarajia katika mwaka wa bajeti unaokuja 2025/2026 bajeti ya *TARURA* itakuwa ni shilingi trilioni 1.18.

Mheshimiwa Spika, katika wilaya hii, katika Jimbo hili la Vunjo katika kipindi cha miaka minne tayari zaidi ya shilingi bilioni 10 zimetumika kwa ajili ya kuendeleza miundombinu ya barabara hizi za wilaya, lakini katika mwaka wa fedha unaokuja tayari tunatarajia tutakuwa tuna shilingi bilioni 4.6 kwa ajili ya kuendelea kuimarisha mtandao wa barabara hizi za *TARURA*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Zuena Bushiri kwamba kama vile Serikali ambavyo imekuwa

ikitenga fedha kila mwaka wa bajeti kuanzia mwaka 2019/2020, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha inakamilisha barabara hii ya Uchira – Kisomachi kwa kiwango cha lami katika Jimbo la Vunjo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona. Maswali kwa kifupi, moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Dkt. Kimei, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwa moyo wa dhati ninaomba nitoe shukrani nyingi kwa Mheshimiwa Mchengerwa, Waziri wa TAMISEMI kwa kutembelea Jimbo la Vunjo, hususani Barabara ya Chekereni – Kahe – Mabogini na kutoa maagizo chanya kuhusiana na ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri, je, kazi hiyo itaanza lini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwa hakika Mheshimiwa Dkt. Kimei amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara hizi za wilaya katika jimbo lake inaendelea kuimarishwa. Ninakumbuka mwaka 2024 alileta timu hapa ya watu kutoka jimboni kwake, tukakaa pamoja ofisini kujadili na kutengeneza mipango.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema yeye mwenyewe hivi karibuni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, alifika katika Jimbo la Vunjo kwenye ziara na akaagiza kwamba Barabara hii ya Chekereni – Kahe – Mabogini iweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimuhakikishie Mheshimiwa Dkt. Kimei, kwamba, tayari sisi kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI tukitumia uratibu wa Mameneja wetu wa *TARURA* katika ngazi ya

mkoa na wilaya tumeanza taratibu kwa ajili ya kuanza kutekeleza maagizo haya ya Mheshimiwa Waziri. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, barabara hii itajengwa ili wananchi wako waweze kupata barabara nzuri ya kufanya shughuli zao za kiuchumi na kufikia huduma muhimu za kijamii.

**SPIKA:** Waheshimiwa narejea tena, maswali kwa kifupi bila historia. Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, eneo la Mpamaa - Msalato, walikuwa wanachonga zile barabara za mitaa. Ni lini sasa mtamalizia kujenga barabara za mitaa katika eneo lile la Mpamaa - Msalato ili wananchi wafike kwenye makazi yao? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kuhakikisha kwamba inaongeza mtandao wa barabara hizi za wilaya ambazo zina umuhimu mkubwa sana kiuchumi, lakini zinaweza kuwasaidia wananchi kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Serikali imeanza kuchonga barabara katika eneo la Mpamaa – Msalato na ninaomba nitumie nafasi hii kuendelea kumsisitiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa na wa Wilaya, wasimamie kwa ukamilifu zoezi hili ili liweze kukamilika nab bb hizi ziweze kufunguka ili wananchi waweze kuzitumia kwa manufaa mapana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Barabara ya Jaribu – Mpakani, Kivinje – Nanjache yenye urefu wa kilometa 32 ujenzi wake umesimama, mkandarasi hayupo *site* na muda wa ujenzi ulishakwisha. Ni nini kauli ya Serikali juu ya kadhia hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kumkumbusha Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Pwani pamoja na Meneja wa *TARURA* ngazi ya Wilaya waweze kufanya ufuatiliaji wa karibu kabisa ili waweze kujua changamoto ni nini ambayo inafanya mkandarasi asiwepo *site*, lakini waweze kuamua changamoto iliyojitokeza. Wawasiliane na sisi kama kuna changamoto ambayo iko juu ya uwezo wao ili tuweze kuikwamua barabara hii iweze kujengwa na mkandarasi arudi *site*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KEHANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, Barabara ya Namanyere – Mashete imekuwa na changamoto kwa muda mrefu. Ni upi mkakati wa Serikali wa kuikarabati kwa sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikitenga bajeti kwa kila mwaka wa fedha kwa ajili ya kuhakikisha inaendelea kuimarisha barabara hizi za wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Ni dhahiri kabisa utaona kuna ongezeko la bajeti. Tangu Serikali ya Awamu ya Sita ilipoingia madarakani ilikuta bajeti ya *TARURA* kwa mwaka ni shilingi bilioni 275, lakini hivi tunavyozungumza tunatarajia bajeti ya *TARURA* katika mwaka wa fedha 2025/2026 itakuwa ni shilingi trilioni 1.18.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Aida Khenani, kwamba barabara hii katika eneo hili la Namanyere itajengwa ili iweze kuwanufaisha wananchi wako na waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi, lakini waweze kufikia huduma za kimsingi za kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza ninaipongeza Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kutujengea kilometa 33 ya barabara kutoka Iringa Mjini kupitia Kalenga kwenda Kilolo. *(Makofi)*

Sasa barabara ya kutoka Mtandika kwenda Nyanzwa ambayo ni kilometa 40; ni lini mtaijenga hata kwa kiwango cha changarawe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri Mheshimiwa Grace Tendega anaona kazi kubwa inayofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha barabara zetu hizi (mtandao wa barabara za *TARURA)* ambazo ni muhimu sana kiuchumi na zinawawezesha wananchi kufikia huduma za kimsingi za kijamii.

Mheshimiwa Spika, kama vile ambavyo umeshuhudia Serikali imekuwa ikifanya kazi kubwa ya kuimarisha mtandao wa barabara hizi za *TARURA,* naomba nikuhakikishie kwamba Barabara hii ya Mtandika kwenda Nyanzwa itaweza kujengwa katika hadhi nzuri. Serikali itafika ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata miundombinu mizuri ya barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, Mbunge wa Donge, sasa aulize swali lake.

Na. 353

### *NEMC* Kuishirikisha *ZEMA* katika Miradi Zanzibar

**MHE. MOHAMMED JUMAH SOUD** aliuliza: -

Je, kwa nini *NEMC* haianzishi utaratibu wa kuishirikisha *ZEMA* ili kuongeza ufanisi wa uibuaji na usimamizi wa miradi ya mazingira Zanzibar?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza ufanisi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumekuwa na utaratibu wa kushirikiana kati ya *NEMC* na *ZEMA* katika uibuaji na usimamizi wa miradi ya mazingira. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali zikiwemo hatua za maandalizi na utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa mradi unaotekelezwa ni mradi wa kuimarisha uwezo wa jamii za pwani kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu unatekelezwa Unguja na Pemba kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni moja. Aidha, miradi miwili inayoandaliwa kwa ushirikiano wa *NEMC* na *ZEMA* ni kama ifuatavyo: -

(a) Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yenye upungufu wa maji baridi; mradi huu upo katika hatua za kupata kibali cha fedha kutoka Mfuko wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi - *Adaptation Fund* na utatekelezwa Unguja na Pemba kwa thamani ya dola za Kimarekani milioni 3.5.

(b) Mradi wa kuimarisha miundombinu katika ukanda wa pwani ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi; mradi huu upo katika hatua za kupitishwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika na utatekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar, nakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohammed Jumah Soud, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMMED JUMAH SOUD:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali namba moja; kwa kuwa mwongozo wa ushirikiano kwa taasisi ambazo siyo za Muungano unazielekeza taasisi ambazo siyo za Muungano kuweza kukutana angalau mara moja katika kila robo mwaka. Je, taasisi hizi za *ZEMA* na *NEMC* katika mwaka huu wa fedha wa 2024/2025 zimeshakutana mara ngapi na matokeo yake katika vikao hivyo ni matokeo gani?

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili; nilikuwa nataka kujua, kwa kuwa hizi *NEMC* na *ZEMA* ni watoto pacha, mmoja anafanya kazi Tanzania Bara na mmoja anafanya kazi zake Visiwani, ni ndugu hawa.

Mheshimiwa Spika, je, ni miradi mingapi ambayo ameshaitayarisha ambayo inakwenda kutekelezwa na kwa kipindi kilichopita miradi mingapi ambayo imeshapatiwa fedha ambayo wanaitekeleza kwa pamoja *ZEMA* na *NEMC*? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri maswali yake yanahusu takwimu, kama unazo takwimu unaweza kumpa Mheshimiwa Mbunge, lakini kama huna, kanuni zetu zinakuruhusu kumpatia takwimu baadaye.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, niridhie tu kwamba

niombe baadaye nifafanue niweze kupata takwimu sahihi ili niweze kumpatia Mheshimiwa Mbunge, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Zanzibar walishakuwa na Mamlaka ya Mazingira na Uhifadhi, je, ni lini *NEMC* nao watapata mamlaka kama hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Zanzibar wanayo Mamlaka ya Mazingira inaitwa *ZEMA*, lakini kwa upande wa huku Tanzania Bara tunayo *NEMC* ambayo bado ni Baraza, nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mchakato wa kuifanya *NEMC* kuwa *NEMA* kwa maana ya kwamba kuwa na mamlaka, mchakato huu umeshaanza na nimwambie tu kwamba wakati utakapofika mchakato huu utafika kwenye Bunge lako Tukufu na tutaujadili kwa pamoja ili lengo na madhumuni tuweze kuipa nguvu zaidi *NEMC* iweze kuwa na mamlaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simai, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini *NEMA* na *ZEMA* zitakuwa na ushirikiano wa pamoja ili kwenda kuondosha changamoto za maji ya bahari yanayoweza kuvamia maeneo ya makazi maeneo ya Kaskazini Unguja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwa kuna changamoto sasa ya athari ya mabadiliko ya tabianchi maji ya bahari yanatoka kwenye kina na yanaingia kwenye makazi na

mengine yanakwenda kuathiri kwenye maeneo ya vipando ambavyo havistahimili maji ya chumvi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ambayo tuliiwasilisha hapa tuliisoma na Wabunge hawa wakaipitisha tarehe 25 Aprili, mwaka huu ya 2025/2026 moja ya miongoni mwa mambo ambayo tumesema tutayapa kipaumbele ni kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua changamoto ya maji ya bahari yanayoingia kwenye makazi ikiwemo maeneo ya Nungwi, maeneo ya Sepwese, maeneo ya Mgando, maeneo ya Mtwara na maeneo yote ambayo yanatoka maji ya bahari na yanaingia kwenye makazi.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa awe na subira kazi hii inakwenda kuanza hivi karibuni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mbunge wa Arumeru Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 354

**Ukarabati wa Mnada wa Olokii Arumeru Magharibi**

**MHE. NOAH L. SAPUTU** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati Mnada wa Olokii uliopo Kata ya Bwawani – Arumeru Magharibi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inawajibu wa kuhakikisha kuwa biashara ya mifugo inafanyika katika mazingira yenye miundombinu muhimu ili

kurahisisha biashara hiyo. Aidha, Mnada wa Olokii uliopo katika Kata ya Bwawani, Arumeru Magharibi ni mnada wa upili unaosimamiwa moja kwa moja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na mnada huu hufanya kazi kila Ijumaa ya wiki.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa mnada huo Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ipo katika taratibu za umiliki wa eneo la mnada huo na mara tu taratibu hizo zitakapokamilika Serikali itakua tayari kufanya ukarabati wa mnada huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza kwa kuwa nimeuliza swali hili leo ni mara ya tatu, mara ya kwanza majibu yalikuwa ni itawekwa kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023, mara ya pili ilikuwa itawekwa kwenye bajeti ya mwaka 2023/2024; lakini leo majibu yaliyokuja ni kwamba wanatafuta hati. Mnada huu umemilikiwa tangu mwaka 1968 - 1970; je, nini kauli ya Serikali kuhusu majibu haya ambayo hayaendani ambayo yameelezwa pia hapa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Wizara inakusanya fedha tangu mwaka 1968 - 1970 na mpaka sasa na pale kuna changamoto ya choo, hakuna maji na miundombiinu mingine kama uzio wa mifugo; nini kauli ya Serikali kwamba kutumia fedha ambazo wanazikusanya kwenye mnada huo ili waweze kuweka miundombinu hiyo hasa choo na maji kwa wakati huu wa dharura?

**SPIKA:** Mheshimiwa Saputu umesema haya majibu hayaendani na swali au ni kwamba majibu yanaendana na swali ila umeshajibiwa hivyo mara kadhaa ili nijue kama maswali yako ya nyongeza yajibiwe au hapana.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nimesema niliuliza swali hili kwa mara ya tatu leo, lakini jibu lililokuwa la kwanza ilikuwa lipo kwenye bajeti ili ukarabatiwe, lakini jibu la leo

limekuja tofauti kwamba wanatafuta mpaka wapate kibali ndiyo waweze kufanya ukarabati.

**SPIKA:** Sawa, mimi nataka kujua hili jibu kwanza maana ili uulize swali la nyongeza lazima majibu yaliyopo hapa uwe unakubaliana nayo. Sasa haya majibu hapa unakubaliana nayo ili nimpe nafasi ya kujibu ya nyongeza, kama hukubaliani nayo maana yake ndiyo tuanze kutafuta sasa wewe ulikuwa unatafuta nini hapa kwenye swali lako.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, yanaendana kwa sababu si wamesema wanatafuta hati.

**SPIKA:** Basi sawa. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nimuondoe shaka Mheshimiwa Noah Saputu, Mbunge wa Arumeru Magharibi kwamba majibu yote ambayo Serikali tumekuwa tukiyatoa tunayatoa kwa usahihi kwa sababu lengo letu ni kuhakikisha kwamba taratibu zote tunafata ili mnada huu uweze kukamilika na nimthibitishie tu kwamba changamoto chache ambazo zipo katika eneo hilo kama ujenzi wa choo, upatikanaji wa maji ni sehemu ya zile changamoto ndogo ambazo tumekuwa tukizitatua, lakini sisi tunataka Wizara ya Mifugo kufanya ule ukarabati mkubwa ambao utahusisha soko zima. Kwa hiyo, ule ukarabati mkubwa ndiyo unahitaji sasa umiliki wa eneo ndiyo kitu ambacho kikubwa tumekizungumzia.

Mheshimiwa Spika, haya matokeo ya ukarabati mdogo mdogo sijui kama choo kimejaa, maji ya mara moja, hayo yamekuwa yakifanyika na nimthibitishie tu Wizara ya Mifugo italifanya hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mabula nimekuona, lakini anajibu kwa niaba ya Wizara siyo Wizara yake, kwa hiyo kidogo inaleta wasiwasi na majibu, siyo majibu yatakayotoka, lakini kwa sababu siyo Wizara yake basi tumpe nafasi yeye akaketi. Mheshimiwa

Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 355

**Wanaopata Mimba Kutokana na Kubakwa**

**MHE. FATMA H. TOUFIQ** aliuliza: -

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu wasichana waliopata mimba kutokana na kubakwa na wanaopewa mimba na baba zao na ndugu wa karibu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake wa Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ubakaji ni kosa la jinai kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sheria ya Mtoto, Sura Na.13 pamoja na sheria nyingine zinazopinga ukatili kwa watoto. Serikali kupitia Wizara tunayoisimamia inakemea vikali tabia ya ubakaji na ulawiti wa watoto pamoja na matamko na hatua za kisheria ambazo zimekuwa zikichukuliwa, Serikali imeendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto Awamu ya pili wa mwaka 2024/2025 hadi 2028/2029 ambapo umejikita katika kumaliza ukatili ukijumuisha kubakwa na kupewa mimba kwa kuzini na maharimu au ndugu na jamaa wa karibu ikiwemo baba wa kuzaa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Fatma Toufiq swali la nyongeza.

**MHE. FATMA H. TOUFIQ:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu mazuri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, baadhi ya wahanga wa ukatili huu wamekuwa wakijaribu kutoa mimba hizi baada ya kupewa mimba na maharimu wao na hivyo kugharimu maisha yao; je, Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na jambo hili?

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inawasaidiaje wale wahanga wa ukatili ambao wamepewa mimba na maharimu wao na familia zao zimekuwa zikiwatenga? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza Serikali inatoa kauli kali kwa wale wote ambao wanapata mimba na kuzitoa. Kwanza utoaji wa mimba ni kosa la jinai Serikali itaendelea kutoa elimu kupitia maafisa wetu wa ustawi wa jamii kuwaelimisha wahanga wote waliopatwa na changamoto za kupata mimba ili waweze kuondokona na msongo wa mawazo na kupata huduma stahiki.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Serikali inaendelea kutoa huduma za nyumba salama kwa wahanga ambao wametelekezwa na familia zao, lakini inatoa huduma za afya ya mkono kwa mkono, lakini pia tunatoa huduma za msaada kisheria kwa wahanga hao ili kuhakikisha kwamba wanakaa salama na wanaondokana na misongo ya mawazo na kuendelea na maisha yao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, watoto wengi wanaopata mimba za utotoni ni wale watoto ombaomba wa mitaani, je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalinda watoto hawa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango na ina mkakati wa kuwalinda watoto hawa kwa kuwafuata na kuwahoji baadaye baada ya kuwahoji kwa kuwakutanisha na wazazi wao ili waendelee na maisha na wazazi pale wanaposhindwa basi Serikali ina vituo vyetu vya kulelea watoto ambapo vipo Dodoma, lakini vipo Dar es Salaam na watoto hao wanalelewa na kupata stahiki zote kuanza elimu mpaka wanapokuwa na kutimiza miaka 18 na kuendelea na maisha yao, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 356

**Muswada wa Sheria Kuwalinda Watoto wa Kike**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta muswada wa sheria kuwalinda watoto wa kike wanaofanyiwa vitendo vya usagaji nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Julai, 2023 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipokea taarifa ya Tume ya Kuangalia namna ya Kuboresha Taasisi za Haki Jinai ambapo miongoni mwa mapendekezo ilikuwa

ni kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali za haki jinai ikiwemo Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza mapendekezo ya Tume na hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Haki Jinai *(The Criminal Justice (Miscellaneous Amendment) Bill)* ambapo kifungu cha 176 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kimependekezwa kufanyiwa marekebisho ili kudhibiti vitendo vya ukiukwaji wa maadili ikiwemo vitendo vya usagaji kwa watoto wa kike.

**SPIKA:** Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, swali la nyongeza.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza kabisa niipongeze Serikali kwa kufuatilia kwa undani vitendo hivi ambavyo ni kinyume cha maadili, lakini pia kiimani, lakini pia kisayansi; nina maswali mawili mafupi ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali itachukua muda gani hadi kuleta marekebisho haya ya sheria Bungeni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wakati tunaanda kuleta sheria hii au marekebisho haya ya sheria je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kushirikisha wadau mbalimbali ili waweze kuanza kutoa elimu kwa jamii yetu ili kuondoa suala hili bovu katika jamii yetu la kimaadili, kisayansi na kiimai?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Najma kwa pongezi alizozitoa kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza tutatumia muda gani. Kama nilivyosema tayari Muswada huo tumeshauandaa, kinachosubiriwa ni kwamba twende kwenye uchaguzi, Mungu atujalie turudi tena katika Bunge hili Tukufu na muswada huo utakuwa mezani ili watoto wa kike waweze kupata haki yao kama ambavyo Mheshimiwa Najma anawapigania.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu elimu, kupitia mpango wa msaada wa Kisheria wa Mama Samia Serikali imekuwa ikitoa elimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, asasi za kiraia na taasisi nyingine mbalimbali, katika elimu hiyo tunatoa elimu pia za haki za binadamu, haki za wanawake, haki za wasichana ambapo jambo hili nalo linatolewa elimu kwa kiwango kikubwa sana na tunaamini kwa kuwa tumeenda vizuri katika awamu ya kwanza ya mpango huo tutaendeleza katika awamu ya pili ili tutokomeze kabisa jambo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Mwikabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ili upambane na wahalifu inabidi wewe usiwe sehemu ya wahalifu, sasa ili Watanzania na hasa Bunge tupigane vita ya usagaji na ushoga; je, Serikali ipo tayari kuweka masharti hapo na mashine hapo nje Wabunge wote wanapoingia humu ndani wapimwe kwanza tujue kama kuna usagaji na kama kuna mashoga ili tupambane na ushoga nchi hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, hilo swali linaelekezwa kwa Mheshimiwa Waziri au kwangu?

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, hilo swali linaenda kwa Serikali kwa maana ya Mheshimiwa Waziri wa Sheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa Serikali inaweza kuleta mashine hapa ya kupima kweli Bungeni si itakuwa inatuingilia?

Sawa, sasa kama swali lilikuwa linaelekezwa kwangu mimi siwezi kuulizwa swali nikiwa hapa mbele. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri pia hilo swali kwa kuwa halikuhusu wewe kwa hiyo hilo sitakupa nafasi ya kulijibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Angelina Malembeka, swali la nyongeza.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kufahamu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri katika huo muswada wanaouandaa kwa ajili ya wanawake kwa suala la usagaji; je, wamezingatia kwenye suala la ulawiti kwa sababu sasa hivi suala la ulawiti ni kubwa zaidi kuliko hilo la usagaji? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, Sheria ya Makosa ya Jinai, Sura 16 ilifanyiwa mabadiliko makubwa mwaka 1998 kupitia Sheria Namba 4 ya mwaka 1998 ambapo makosa mengi ya kujamiiana yaliingizwa mule ikiwemo kosa la ulawiti. Hili kosa tunalolisema hapa ni kosa ambalo halikuingizwa katika mabadiliko ya mwaka 1998 na ndiyo maana tunapendekeza liingizwe sasa. Hivyo basi suala la ulawiti tayari lipo kwenye sheria zetu kwa hivi sasa, kinachotakiwa ni elimu na utekelezaji wa sheria iliyopo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 357

**Kutoa Dawa Bure kwa Wagonjwa wa Akili**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:-

Je, nini mkakati wa Serikali kutoa dawa bure kwa wagonjwa wa akili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali wa utoaji wa huduma za afya unafuata Sera ya Afya ya mwaka 2007, Sura ya 5 sehemu ya 4 Ibara ya 1 hadi 3 ambayo imefafanua njia mbalimbali za ushirikishaji, uchangiaji na utoaji misamaha ya huduma za afya. Sera inaelekeza wagonjwa wenye magonjwa ya muda mrefu ikiwemo matatizo ya afya ya akili wanaweza kupatiwa msamaha wa huduma za matibabu kulingana na uwezo wa wagonjwa hao au watu wanaowahudumia kupitia mifumo inayohusisha Afisa Ustawi wa hospitali na watendaji kutoka eneo ambalo mgonjwa anaishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini njia zilizoelezwa kwenye jibu la msingi hazinufaishi walengwa ipasavyo. Nini kauli ya Serikali kwa hili?

Mheshimiwa Spika, pia kupitia Bunge lako Tukufu Serikali inaonaje ikawakumbusha Maafisa Ustawi kutekeleza haya ambayo yameelezwa kwenye jibu la msingi kwa kuwa tayari tuna takwimu sahihi za watu wenye ulemavu. Hali ya wagonjwa wa akili si nzuri na hasa ikizingatia kwamba hawana uwezo wa kugharamia matibabu haya naomba kauli ya Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Stella Ikupa, kwanza nianze kwa kumpongeza, kwa sababu kwa kweli kama kuna eneo ambalo ametendea haki katika Bunge hili kwa miaka hii mitano ni eneo hili la walemavu, lakini pia la wenzetu wenye matatizo ya akili.

Mheshimiwa Spika, mimi nimwambie tu kwa sababu tunakuja na sera mpya ya afya, eneo hili tutaenda kuliangalia kwa kina tuone ni namna gani tunaweza tukaboresha na mimi na

wewe tushirikiane ili utupe mawazo tuweze kuja na namna nyingine nzuri mpya ambayo inaweza ikawafikia vizuri wahusika.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni kwamba niwaambiaje Maafisa Ustawi wa Jamii ili waweze kufanya kazi yao. Mimi niseme tu, nisisitize tu, moja; kuwaomba wananchi ambao wana wagonjwa wa aina mbalimbali wasiyo na uwezo wa kulipa, washirikiane na Watendaji wa Kata kuhakikisha wakati wanaelekea kwenye hospitali basi wawe tayari na zile barua za Watendaji wa Kata na kuwaomba watendaji wa kata nchi nzima watoe ushirikiano kwa wagonjwa na ndugu wa wagonjwa ili kuweze kusaidiwa.

Mheshimiwa Spika, ila nimtoe wasiwasi dada yangu Stella Ikupa, kwa mfano kwenye Hospitali yetu ya Milembe kwa mwaka huu tu kuanzia Juni, 2024 mpaka sasa Serikali imepeleka dawa zenye thamani ya shilingi bilioni 1.72; lakini zaidi ya dawa za shilingi milioni 800 zimetolewa kwa wagonjwa wenye matatizo kama hao ambao hawawezi kujilipia, lakini nikuhakikishie kwamba tutaendelea kuboresha na hili eneo tunachukua na tunaenda kulifanyia kazi ili kutizama kwa kina zaidi kuhakikisha tunaondoa matatizo unayoyasema.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, watoto ambao wana magonjwa ya kifafa na magonjwa mengine kama hayo ambayo yanaathiri ubongo, gharama za kununua dawa zao ni ghali, lakini pia ni za kutumia muda mrefu, wazazi wengine wanaweza kununua za mwaka mmoja miaka mingine mitano wanawaachia katikati.

Je, Serikali haiwezi kutoa ruzuku ku-*suppliment* hizi dawa ili wazazi waweze kununua na watoto waweze kutibiwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, cha kwanza, kwa sababu sasa tulichonacho kwenye Sera ya Afya ni utaratibu huu niliyoutaja hapa, tutaendelea kuuboresha ili uweze kuwafikia na kusaidia watu kama hao, lakini nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge amefanya kazi nzuri sana hapa ya kuja na Bima ya Afya kwa Wote. Mimi nafikiri nalo hili ukijumlisha hili la kisera, pia Bima ya Afya kwa Wote inaweza ikatusaidia tukafika mahali pazuri sana pa kuhudumia watu kama ambavyo ametegemea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Amandus Chinguile, swali la nyongeza.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, wako wananchi wenye tatizo la afya ya akili na bado hawajapata huduma na hasa jamii zetu ni kama vile zimewatenga hasa maeneo ya vijijini. Upi mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba elimu inatolewa na kuhakikisha wale wenye tatizo la afya ya akili tunawafikia na hasa maeneo ya vijijini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, tuna wagonjwa wenye afya ya akili na mara nyingi jamii imeshindwa kusaidiana na Serikali kuhakikisha wanafika kwenye maeneo wanayoweza kupata huduma. Sisi ambacho tunakifanya kwa kushirikiana na TAMISEMI, lakini pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Jamii ni kuendelea kuelimisha jamii ili kutambua haya mambo na kuweza kung'amua hao watu na kuwafikisha mapema kwenye vituo vyetu na kwa kweli jamii imejitahidi.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kwa mwaka huu tu toka Juni mpaka sasa wagonjwa 2,700 wamefikishwa kwenye Hospitali yetu ya Milembe, maana yake hao tu ni wale unaozungumzia Hospitali ya Taifa, maana yake hata kwenye wilaya zetu na sehemu zingine wamefika wengi sana. Kwa hiyo, hamasa imeongezeka, lakini ni kweli bado kuna tatizo tutaendelea kuongeza nguvu kwenye eneo hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, katika zahanati mbalimbali hapa nchini kuna upungufu mkubwa wa dawa, nini kauli ya Serikali kuhakikisha dawa zinapatikana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli, kwa kweli Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshafanya kazi yake kwa maana ya kutoa fedha za kununua dawa na kama kwenye zahanati zetu na kwa kweli najua kwamba nilikuwa nafuatilia *data* za kuanzia taifani kushuka chini ukija kwenye hospitali zetu za zahanati, wilaya utakuta upatikanaji wa dawa ni 88%, kwenye Hospitali za Taifa 99%, 97%, ni kweli kuna upungufu kwa maana kuna 22% ya watu wasiopata dawa. Kikubwa tutaendelea kushirikiana na wataalamu wetu na kuwaonesha namna ya kufanya maoteo vizuri ili wanapoagiza dawa wahakikishe dawa wanazozihitaji wananchi kwenye eneo husika zinapatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 358

**Kukarabati Miundombinu ya Hospitali ya Kitete**

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali wa kukarabati miundombinu ya Hospitali ya Kitete yenye miaka zaidi ya 100?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya mpango wa matumizi ya ardhi *(master plan)* unaotoa mwongozo wa uboreshaji wa Hospitali ya Kitete tayari umekamilika. Hatua inayofuata ni kuanza utekelezaji wa ujenzi wa jengo jipya la wagonjwa wa nje *(OPD)*.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, majengo katika hospitali ile mengi ni tangu wakati wa mkoloni yalikuwa yanatumika kama kambi ya jeshi, ndiyo maana nimeiomba Serikali, lini mtakarabati majengo yale na siyo ujenzi wa jengo la *OPD*, mtakarabati majengo yale ili yaweze kufanana na Hospitali ya Mkoa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, ujenzi wa jengo la *OPD* kwenye hospitali ile, mnaendelea kuongeza msongamano kwenye eneo lile kwa sababu ni dogo na halitoshi kuendelea kuweka majengo mengine. Serikali haioni haja sasa ya kutengeneza bajeti ili kuweza kujenga Hospitali Mpya ya Mkoa wa Tabora itakayoendana na hadhi ya mkoa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nijibu maswali ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, moja; najua yeye amekwenda pale kwenye hospitali na anajua miezi minne iliyopita nilikuwepo pale, ukiingia pale kwenye Hospitali ya Kitete utaona kuna ujenzi umeanza upande mwingine, ukiingia tu utaona ujenzi umeanza lakini tumekwambia hapa kuna *master plan. Master plan* hii yote siyo tu suala la kukarabati yale majengo, tunataka yabomolewe halafu tunyanyue majengo ya kwenda juu ili sasa watu waweze kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, Mbunge alitamani kwamba ile hospitali iweze kujengwa sehemu nyingine badala ya kujenga eneo lile, labda nikuombe Mheshimiwa Mbunge kwa sababu ili kuamua hilo ni lazima kushirikiana wewe, lakini kwa maana ya *RCC* ya Mkoa wako na makubaliano ya maendeleo ya mkoa wako, hebu tushirikiane kwa pamoja wakati tuna hii *master plan* haijaanza kutekelezwa, ili tutakapokuja na mkakati wa pamoja na Mkoa wa Tabora, ninyi mtakachokisema kama mkoa basi tutaenda nacho kwa pamoja kama *plan* yetu ya pamoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itajenga ukuta kwenye hospitali ya Wilaya ya Longido ili kulinda faragha za wagonjwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo anasema Mheshimiwa Mbunge, ni kweli Hospitali ya Wilaya ya Longido imekaa na iko sehemu ambayo ni kubwa ya uwazi mkubwa na ni *open,* nitakachofanya tutashirikiana na wenzangu wa TAMISEMI ili kuona ni namna gani wanaweza wakaweka suala hilo la ukuta kama mojawapo ya kipaumbele baada ya kumaliza majengo ya msingi ndani ya hospitali hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Mji wa Bunda kwenye Jimbo la Bunda Mjini tunajenga hospitali yetu ya halmashauri kwenye Kata ya *Bunda Stoo*, mwaka jana zilikuja shilingi milioni 800 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi baadaye zikarudi. Hivi sasa ujenzi umesimama; ni lini mtatupa hizo pesa ili tuendelee na ujenzi na wananchi wa Bunda wapate huduma ya afya bora?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ngoja, hilo ni la kwako au ni la TAMISEMI? Ni la TAMISEMI?

Naibu Waziri TAMISEMI, Mheshimiwa Dugange, anauliza lini pesa za kumalizia ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Bunda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bulaya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali ilishapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda na tayari baadhi ya majengo yamekamilika na yameanza kutoa huduma, lakini ilikuwa ni awamu ya kwanza na ya pili. Ujenzi wa majengo ya hospitali za halmashauri unakwenda kwa awamu na tutakwenda awamu ya tatu ambayo itakamilisha kwanza majengo ambayo hayajakamilika, lakini pili tutaanza kujenga majengo mengine ambayo yalisalia katika ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi la ujenzi ni la awamu na tutahakikisha kwamba tunakamilisha majengo hayo kwa wakati.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Esther Edwin Malleko, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 359

**Kuboresha Miundombinu ya Maji Safi kwa Wakazi wa Kilimanjaro**

**MHE. ESTHER E. MALLEKO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha miundombinu ya maji safi na salama kwa wakazi wa Kilimanjaro?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa Mkoa wa Kilimanjaro ni wastani wa 88% vijijini huku eneo la Mji wa Moshi likiwa linapata huduma kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha huduma ya maji mkoani Kilimanjaro, Serikali katika mwaka wa fedha 2024/2025 imekamilisha utekelezaji wa jumla ya miradi 13 ukiwemo Mradi wa Maji Same-Mwanga-Korogwe. Aidha, Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi mingine 11 ya Kiluwio, Vuje, Mroyo-Kisangaze, Msindo, Kirangare (Same), Kileo Kivulini (Mwanga), Endumenti (Rombo), Marangu (Moshi), Kikafu-Kwa Sadala, Losaa-KIA (Hai) pamoja na mradi wa vijiji nane katika Wilaya ya Siha. Miradi hiyo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na itakapokamilika inategemewa kuboresha huduma ya maji safi na salama Mkoani Kilimanjaro.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Malleko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali lakini bado kuna changamoto kwenye Kata za Mamba Kusini, Mwika Kusini na Mwika Kaskazini ambapo mpaka sasa kuna uhaba mkubwa wa maji. Tumepata kiwanja katika Kata ya Mwika Kaskazini kwa ajili ya kuchimba kisima, lakini mpaka sasa *MUWASA* wameomba fedha takribani miaka miwili sasa hawajaweza kupatiwa ili waweze kuchimba kisima hicho.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha inapambana na upotevu mkubwa wa maji ambao unaendelea kuipa hasara Wizara hii?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Esther, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa tumekuwa tukishirikiana na Mheshimiwa Mbunge katika baadhi ya maeneo ambayo ameona yana changamoto, amekuwa akiyaleta na sisi kama Serikali tumeendelea kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amewekeza takribani shilingi bilioni 10.14 kwa Mkoa wa Kilimanjaro kwa ajili ya miradi 15, vilevile tunaelewa kabisa kwamba kati ya vijiji 12,318 nchi nzima, tayari tumeshafikia vijiji 10,500 ambavyo tayari vimeshafikiwa huduma ya maji safi na salama.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kushirikiana kama ambavyo amekuwa akiwasemea zaidi Wana-Kilimanjaro nami nitaendelea kumpa ushirikiano kwa niaba ya Serikali ili tuhakikishe kwamba vijiji vya Mamba Kaskazini, Mwika Kaskazini na Mwika Kusini vyote vinaingizwa katika mpango wa kufikishiwa huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa swali la upotevu wa maji, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba tunaendelea kupunguza upotevu wa maji kwa sababu ni hasara kubwa kwa Serikali tunapowekeza, pia ni gharama kubwa kwa watumiaji pale ambapo tunazalisha kwa gharama kubwa, lakini maji yanapotea, watumiaji kule wanajikuta wanagharamika gharama za uzalishaji wakati maji hayawafikii.

Mheshimiwa Spika, sisi Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba tunaboresha miundombinu lakini katika *designing* zetu tuhakikishe kwamba tuna *design* ambazo hazisababishi upotevu wa maji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ni mpango wa Serikali, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewaona, lakini maswali mafupi, narejea tena.

Mheshimiwa Mussa Sima, swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ni upi mkakati wa Serikali kuhakikisha Mradi wa Miji 28 unakamilika kwa wakati pale Singida Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kwanza kabisa kwa miradi yote ya Miji 28 ikiwemo na Singida Mjini ni kukamilika ndani ya mkataba ambao tumeingia na wakandarasi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Godwin Kunambi, swali la nyongeza.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Ni lini mradi wa maji wa Tarafa ya Mlimba utakamilika? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Mradi wa Mlimba ulikuwa na changamoto kidogo kwa sababu ya mabomba kadhaa na kulikuwa na ucheleweshaji kidogo wa malipo, lakini sasa hivi tayari Serikali imeshakaa na mkandarasi na kukubaliana twende kwa utaratibu gani ili mradi huu ukamilike.

Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mradi huo tunautazama kwa jicho la kipekee kuhakikisha kwamba

unakamilika na watu wake wapate maji safi na salama, ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, shukrani zenu kwa kupewa nafasi nimeshazipokea, kwa hiyo msinishukuru.

Mheshimiwa Abdallah Chaurembo, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatatua tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama katika eneo la Kwa Mwarabu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbagala ni kweli kabisa kuna maeneo ambayo yana chngamoto, siyo Kwa Mwarabu peke yake. Mheshimiwa Mbunge ameshaleta maeneo mengine ambayo tayari tumeshachukua hatua na tumeshamaliza kuyafanyia kazi na hilo tumhakikishie kwamba Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan haitashindwa kwenda kutatua changamoto hiyo ya Kwa Mwarabu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Kichonda, Kijiji cha Kichonda kina tatizo sugu sana la maji na la muda mrefu, lini Serikali itakuja kutatua tatizo hili kwa wananchi wale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Kichonda, Kijiji cha Kichonda Serikali inatambua changamoto iliyopo pale na sisi katika bajeti yetu hii ambayo Waheshimiwa Wabunge waliyoipitisha wiki iliyopita ya shilingi trilioni 1.016

inaenda kutatua changamoto katika Kata ya Kichonda na Kijiji cha Kichonda.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, ipi kauli ya Serikali kuhusu kupeleka maji katika baadhi ya maeneo ya Kata za Mbokomu na Kimochi ambazo tunauhaba mkubwa wa maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Ndakidemi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Profesa Ndakisemi wakati tunapanga bajeti yetu alitufikishia changamoto hii ya Kata hii ya Mbokomu pamoja na Kimochi ili tuweke katika mpango na tayari tumeshaingiza kwenye mpango. Kwa hiyo, tumuombe Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kwa ajili ya kwenda kutekeleza mradi huu, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Halima Mdee, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Makongo Jimbo la Kawe kumekuwa na changamoto ya kupasuka mabomba sana; ni lini tatizo hili litatatuliwa ili wananchi wapate maji kwa uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, sijalisikia vizuri, ahsante.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Makongo, Jimbo la Kawe kumekuwa na tatizo la mabomba kupasuka sana; ni lini tatizo hili litatatuliwa ili wananchi wapate maji kwa uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Mdee, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Kata ya Makongo, ni kwa sababu ya jiografia yake na jiografia hiyo inasababisha maji kutofika katika baadhi ya maeneo na yanapokuwa hayafiki, sasa inabidi tutengeneze *booster station* ambazo zinabidi zi-*pump* maji, sasa kwenye ku-*pump* maji kwa kasi maana yake inasababisha ile *pressure* inakuwa kubwa na mabomba yanapasuka.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa tubnabadilisha uwekaji wa mabonda ya *plastic* tunaweka mabomba ya chuma ili kuhakikisha kwamba hata ule msukumo unapokuwa mkubwa basi tunaweza kuhimili na maji yanaweza kufika kwa wakati bila kuwa na changamoto, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Rwabwere imekuwa na changamoto ya muda mrefu, ni kata nzima vijiji havina maji safi wala salama, nataka kujua ni lini mchakato wa uchimbaji wa visima utakamilika ili wananchi hao waweze kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa programu ya visima 900 na visima hivi vinaendelea kuchimbwa nchi nzima, lakini tunatambua kwamba kuna maeneo mengine ambayo katika visima vitano hivyo kulingana na upendeleo wa Wabunge ambao waliamua wapeleke maeneo fulani, sisi tumechukua changamoto ya *gap* ambalo limeonekana kwamba kuna maeneo mengine bado yatakuwa na uhitaji huo.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tumelichukua na tutahakikisha kwamba kwanza vile ambavyo tumepanga vichimbwe vikamilike kwa wakati, tujenge *point source* maana yake eneo la kutolea huduma, pia na kutengeneza mtandao kwenye visima ambavyo tumepata maji mengi na maeneo ambayo tutabaini kwamba bado yanahitaji huduma ya maji tutahakikisha kwamba tunaenda kuchimba visima au tutaweza kupeleka mtandao wa maji kulingana na kisima ambacho kimeonekana kina maji mengi, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Chereheni, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mradi wa Maji katika Kata ya Igunda sasa takribani miaka minne haujakamilika. Ni nini mkakati wa Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Cherehani wiki iliyopita tu alikuwepo ofisini na tumejadili kuhusu hili suala yale ambayo tulikubaliana Mheshimiwa Cherehani nikuhakikishie kwamba huo mradi tayari tumeingiza kwenye mpango na tutahakikisha kwamba fedha zinaenda tuna majadiliano na wenzetu Wizara ya Fedha watoe fedha ili tuhakikishe kwamba mkandarasi akautekeleze mradi huo na ukamilike kwa wakati kwa niaba ya wananchi wako, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, sasa aulize swali lake. Haya, Mheshimiwa Hawa Mchafu.

Na. 360

**Kukamilika kwa Mradi wa Maji Ndanda**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE** aliuliza:-

Je, lini Miradi ya Maji ya Nambawala, Chiwata, Mbemba, Ndanda na Nanganga itakamilika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imekamilisha utekelezaji wa miradi ya maji ya Nambawala, Chiwata, Mbemba, Ndanda na Nanganga iliyopo Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara. Kazi zilizofanyika katika miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa matanki saba yenye jumla ya ujazo wa lita 950,000, ulazaji wa bomba umbali wa kilometa 85 pamoja na ujenzi wa vituo 34 vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa miradi hiyo inanufaisha zaidi ya wananchi 25,582 waishio kwenye Vijiji 13 vya Nambawala A, Nambawala B, Chiwate, Chibya, Mbemba, Nanganga A, Nanganga B, Umburu, Mkungu, Majengo, Tuungane, Liputu na Njenga.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Hawa Mchafu, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwambe na kufuatia majibu ya Serikali ni kwamba sawa mradi umekamilika, lakini watu wa Ndanda pamoja na Nanganga bado hawajaanza kuyatumia au kuyanywa maji hayo.

Mheshimiwa Spika, sasa ni lini Serikali itahakikisha kwamba watu wanaanza kuyatumia maji haya?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; changamoto ya kutokukamilika kwa mradi iliyopo katika Jimbo la Ndanda inafanana kabisa na ile iliyopo Wilayani Kisarawe katika Kata ya Masaki. Ni lini Kata ya Masaki watapata maji safi na salama? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama Mheshimiwa Mbunge alivyouliza mradi tayari umeshakamilika na hii ni kwa sababu Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imejidhatiti kuhakikisha kwamba miradi mingi inakamilika.

Mheshimiwa Spika, suala la kukamilika maana yake ni utoaji huduma kwa wananchi na hiyo ndiyo dhamira ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, nimtoe hofu kuna baadhi ya vitu vidogo ambavyo vinaendana pia na ubora wa maji ambapo ni lazima kabla hatujayafikisha kwa wananchi tuhakikishe kwamba ubora unaotakiwa basi uwe umefikiwa na ili waweze kupata huduma hiyo ya maji safi na salama. Nimtoe hofu maji wataanza kunywa ya kutoka katika mradi huo.

Mheshimiwa Spika, vilevile mradi huu wa Mkoa wa Pwani ambao Mheshimiwa Mbunge ameongelea. Natambua kabisa kwamba katika Mkoa wa Pwani kuna maeneo ambayo mengi ambayo hayajapata huduma ya maji safi na salama kama ambavyo Mheshimiwa Hawa amekuwa akitueleza sisi Wizara ya Maji na sisi tumeendelea kuyachukua lakini *specifically* katika eneo ambalo umesema tayari liko katika mpango wa bajeti wa 2025/2026 na tuombe tu kwamba utakaporejea tena Bungeni basi utakuwa umepata majibu sahihi kwa ajili ya matumizi ambayo yatakuwa yamepatikana kwa wananchi wa Pwani, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Madini, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Nanyumbu, sasa aulize swali lake.

Na. 361

**Fedha Zilizopatikana Kutokana na Uwepo wa Madini – Nanyumbu**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza:-

Je, fedha kiasi gani zimepatikana kutokana na madini katika Wilaya ya Nanyumbu kuanzia mwaka 2020 hadi 2023?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini Mheshimiwa Dkt. Steven Kiruswa, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Nanyumbu ina jumla ya leseni za uchimbaji mdogo wa madini zilizo hai 66. Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2020 hadi 2023, madini ya dhahabu yenye thamani ya shilingi bilioni 1.28 yalizalishwa. Mauzo ya madini hayo yamewezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi milioni 93.33 kupitia mrabaha, ada ya ukaguzi na ushuru wa huduma *(service levy)*.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini imeendelea kuwaelimisha na kuwasihi wadau wote wenye leseni kuendeleza maeneo yao ya uchimbaji na pia wale wote wenye nia na vigezo wajitokeze kujisajili kupata leseni ili kuongeza uzalishaji na ukuaji wa sekta ya madini katika Wilaya ya Nanyumbu na Mkoa wa Mtwara kwa ujumla, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Yahya Ally Mhata, swali la nyongeza.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; ningependa kufahamu, je, vijiji vinavyohusika na uwekezaji huu vimenufaika vipi na hawa wawekezaji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; nilitaka kufahamu hapo mwanzo Wilaya ya Nanyumbu kulikuwa na ofisi inayoshughulika

na ununuzi wa madini, kwa kipindi kirefu ofisi ile imefungwa hivyo kuleta hali ngumu sana kwa wafanyabiashara. Je, ni lini ofisi ile itafunguliwa ili kuongeza kasi ya mzunguko wa pesa ndani ya jimbo langu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la mchango wa sekta ya madini katika maisha ya wananchi wa Nayumbu ni suala ambalo linaweza likatazamwa katika namna mbili, namna ya kwanza; ingekuwa wachimbaji hawa ni wakubwa wangechangia kupitia ushirikishwaji wa wananchi katika uchimbaji wa madini kwa maana ya kutoa fursa za kutoa huduma, lakini pia kupitia *CSR*.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu ya swali la msingi kwamba hawa ni wachimbaji wadogo mchango wao mdogo unaoingia katika jamii unatokana na watu wanaoajirika kupitia hao wachimbaji wadogo. Wako watu waliopata vibarua, wako akina mama waliotoa huduma na hizo ni huduma ambazo zinatokana na kuwepo kwa uchimbaji mdogo katika katika eneo lile.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili kuhusu ofisi kufungwa na ni lini tutarejesha ofisi hiyo; ofisi za madini au vituo vya kuuza na kununua madini hufunguliwa pale ambapo uchimbaji una tija na unaleta mazao ya kutosha ya madini ambayo yanaleta sababu ya msingi ya kufungua ofisi pale, lakini kwa sababu kama nilivyosema kwamba tunawasihi wenye leseni ambao wako zaidi ya 100 katika eneo la Nanyumbu ambalo leseni nyingine haziko hai, waongeze bidii katika uzalishaji ili tuweze kuzalisha madini ya kutosha kuweza kufungua kituo.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo sisi kama Wizara na kupitia Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan tunaendelea kuhamasisha wawekezaji mbalimbali wajitokeze kwenda eneo la Nanyumbu ili uwekezaji mkubwa wenye tija na kuweza kuruhusu soko lianzishwe pale na liweze kufikiwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Boniphace Butondo, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali iliahidi katika Wilaya ya Kishapu na hasa eneo linalozunguka Mgodo wa Mwadui kwa maana ya Nyenze na Mwanholo kwamba ingetangaza maeneo hayo ili wachimbaji wadogo na wao waweze kupata maeneo ya kuweza kuchimba, lakini mpaka sasa Serikali bado haijatangaza rasmi.

**SPIKA:** Swali.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatangaza sasa maeneo hayo yaainishwe na yaweze kuchimbwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali kupitia Wizara ya Madini kwa sasa ni kufanya utafiti wa awali na wa kina katika baadhi ya maeneo nchini ili kubaini maeneo yenye madini yatakayowawezesha wachimbaji wadogo wanapopewa maeneo wafanye uzalishaji wenye tija.

Mheshimiwa Spika, tunajaribu kuepusha tatizo la kufanya uchimbaji wa kubahatisha na ndiyo maana kwa sasa hivi tunachelea kutangaza maeneo ambayo bado hatujayafanyia utafiti wa kupata uhakiki kwamba kuna uwepo wa madini ili wale wanaopewa zile leseni wasiende kupoteza mitaji yao kwa kuchimba kwa uchimbaji wa kubahatisha.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tutakapokuwa tumepeleka timu zetu za *GST* na *STAMICO* wakafanya utafiti katika yale maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo yatatangazwa kama tulivyofanya katika sehemu zingine nchini ikiwepo hata misitu ya Serikali kule Kigosi ambako tumeshatangaza na kugawa vitalu hata huko kwake pia tutafanya zoezi hilo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Stella Manyanya, swali la nyongeza, moja kwa moja kwenye swali tafadhali.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Nyasa ina uwezo mdogo wa kifedha na kuna malori mengi ya makaa ya mawe yana-*park* barabarani. Je, Wizara itaisaidia Halmashauri ya Nyasa kuweza kusawazisha eneo kwa ajili ya *parking* za malori hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, suala la malori yanayosafirisha mizigo haliko chini ya Wizara ya Madini, nadhani liko chini ya Wizara ya Uchukuzi, lakini kwa sababu Serikali ni moja nitashirikiana na Mheshimiwa Mbunge tuongee na wahusika wa sekta ya uchukuzi waone jinsi ya kuanzisha eneo ambalo litakuwa kama *lorry park* kwa ajili ya kuwezesha utaratibu mzuri wa kupitisha yale madini bila kubughudhi mazingira na wananchi wanaoishi katika maeneo husika.

**SPIKA:** Nadhani alikusudia kwa sababu yale malori yanakuwa yamebeba jambo linalowahusu ninyi basi ninyi ndiyo mchangie hilo eneo la ku-*park* malori na siyo ule uchukuzi kwa maana analizungumzia lori, anazungumzia kilichobebwa kwenye lori. Kwa hiyo, nafikiri ndiyo alitaka kujua ule mchango wa kitu kinachobebwa ndiyo hoja ya Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nimepokea hii hoja, kimsingi tutakwenda kuona namna bora ya kufanya hivyo kwa sababu wanaosafirisha madini tayari wameshatulipa sisi cha kwetu, ule ni mzigo wao na halmashauri huwa na utaratibu wao wa kutoza hela wanapopita katika maeneo husika na fedha hizo zinazoingia kwenye halmashauri ndiyo hasa zingefanya kazi hiyo lakini niko tayari kutoa ushirikiano tuone namna bora ya kusaidia hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Phillipo Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mkoa wa Songwe wa Kimadini ambao makao makuu yako pale Mkwajuni hawana ofisi kabisa za madini. Lini Serikali itajenga Ofisi za Madini Mkoa wa Songwe pale Mkwajuni?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, katika bajeti yetu ambayo imeptishwa wiki mbili zilizopita tumetenga fedha kwa ajili ya kujenga ofisi za madini katika mikoa yote ya kimadini ambayo bado haina ofisi ikiweko Mkoa wa Kimadini wa Songwe.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI**: Mheshimiwa Spika, tunakushukuru kwanza kwa kuja katika eneo la Nyakavangala katika Jimbo la Ismani. Tunazidi kusubiri ahadi ambayo uliwaahidi wachimbaji wadogo wadogo ya kuwapatia vifaa vya uchimbaji pamoja na kupima eneo, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa suala la vifaa vya utafiti na uchimbaji wa madini *STAMICO* imekuwa ikiendelea na zoezi hilo na vifaa vya awali ambavyo Mheshimiwa Rais alivikabidhi kwa wananchi na kanda husika ziligawiwa mwaka juzi mwishoni na tuko mbioni katika kuongeza vifaa vya upimaji madini ikiweko vifaa vya uchorongaji na eneo la Nyakavangala ambalo tumeshalifanyia utafiti wa awali ni moja ya maeneo ambayo tutakapopata mitambo mingine ya kuweka kwenye Kanda ya Nyanda za Juu Kusini nao watakwenda kufaidika kutokana na vifaa hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Lucy John Sabu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 362

**Sekta ya Sanaa na Michezo Kuwanufaisha Vijana**

**MHE. LUCY J. SABU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha sekta ya sanaa na michezo inawanufaisha vijana kwa kuweka mifumo rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imefanya mambo mengi kuhakikisha sekta ya sanaa na michezo inawanufaisha vijana kama ifuatavyo: -

(i) Kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wasanii kupitia Mfuko wa Sanaa na Utamaduni ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi bilioni 5.25 kimetolewa kupitia matawi ya Benki za *CRDB* na *NBC* zenye matawi kote nchini;

(ii) Kurahisisha usajili wa wasanii kupitia Mfumo wa *Artist Information Management System* (*AMIS*) ambao sasa umeunganishwa na ule wa *TAUSI* unaotumiwa na TAMISEMI kwa lengo la kurahisisha zaidi huduma hadi vijijini. Kati ya Julai, 2024 na Aprili, 2025 jumla ya wasanii binafsi 844, vikundi 158, taasisi 39, kampuni 274 na kumbi za burudani 115 zimesajiliwa;

(iii) Kuanzisha Tozo ya Hakimiliki kwa lengo la kuwanufaisha wabunifu wakiwemo wasanii ambapo kati ya mwezi Septemba, 2023 hadi Aprili, 2025, jumla ya shilingi 1,552,751,160 zimekusanywa;

(iv) Kuanza kwa ujenzi wa akademia ya michezo katika chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya kwa lengo la kuibua vipaji hasa kwa vijana wenye umri mdogo; na

(v) Kuendeleza mashindano ya kitaifa ya UMISSETA na UMITASHUMTA kama moja ya njia ya kugundua na kukuza vipaji miongoni mwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

**SPIKA:** Mheshimiwa, Lucy Sabu, swali la nyongeza.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ujenzi wa Chuo cha Michezo Malya na tunashukuru Mheshimiwa waziri Mkuu juzi alikitembelea.

Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha ujenzi wa chuo hicho ili kiweze kuwanufaisha vijana wa Kitanzania na vijana wa Bariadi Mjini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Serikali sasa iko tayari kuhusisha sekta binafsi ili iweze sasa kushiriki kwa lengo la kuboresha na kuibua kwa ajili ya sekta hii ya michezo nchini? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwanza nitambue uwakilishi mzuri wa wanaoupata vijana wa Bariadi Mjini kutoka kwa Mheshimiwa Lucy John Sabu na namtakia kila la kheri kwenye safari yake hii mpya ya kuendelea kuwawakilisha. *(makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la ujenzi wa Kituo cha Michezo cha Malya hata Mheshimiwa Waziri Mkuu amekitembelea Jumapili tu (juzi) na kiko ndani ya muda na

kitakamilika mwishoni mwa mwaka hii mwezi Desemba, 2025 kwa ajili ya kuwawezesha vijana wakiwemo vijana wa Bariadi Mjini kupata maeneo ya kugunduliwa na kutunzwa kwa vipaji vyao. Kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kituo kile ujenzi wake uko ndani ya muda na utakamilika kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ushiriki wa sekta binafsi, katika miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ushiriki mkubwa wa sekta binafsi kwenye masuala ya michezo nchini. Ushahidi unaweza ukaonekana kwa ushiriki wa makampuni kama Azam, Benki ya *NBC*, Benki ya *CRDB,* makampuni ya *GSM*, makampuni ya *MeTL*, *Fountain Gates, Allience Academy* na wengine wengi. Serikali inaendelea kushirikiana na wadau wa sekta binafsi na inaendelea kusimamia mkakati wa utekelezaji wa sera ya maendeleo ya michezo uliotengenezwa hivi karibuni ili kuhakikisha ushiriki wa wadau wa sekta binafsi unaendelea kuwa mkubwa na unaendelea kuchagiza maendeleo ya michezo nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA**: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, je, Serikali ina mpango mkakati gani katika kukuza na kulinda maadili mema kwa wanamichezo na wanasanaa katika uvaaji, mwonekano hata unenguaji ikibidi katika kulinda heshima ya jina la Tanzania yetu na hasa kwa vile wasanii wanafanya vizuri na wanachipukia vizuri? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuwa najaribu kutafakari hili swali namna linavyohusiana na swali la msingi.

Mheshimiwa Asha nafikiri ili tupate majibu mahsusi kwa maswali uliyouliza hebu swali lako ulipeleke kama swali la msingi kwa sababu limetoka kabisa kwenye jambo lililoko hapa, lakini kwa sababu tu aliyesimama ndiyo anayehusika kwa hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri kazi yangu kukulinda Mheshimiwa atuletee kama swali la msingi ili Serikali iweze kujibu kikamilifu swali lako.

Mheshimiwa Festo Sanga swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na changamoto ya migogoro kwenye tasnia ya muziki, lakini tasnia ya michezo kwa maana ya menejimenti za wachezaji na wasanii. Ipi kauli ya Serikali ili kusaidia watu hawa wakue kwenye sanaa kwa sababu tumeona wengine wakipata *depression*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru, masuala ya migogoro kwenye masuala ya mikataba ya kibiashara yanaendelea kushughulikiwa kwa namna ambavyo inastahili.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali kupitia Baraza la Sanaa la Taifa na Baraza la Michezo hali kadhalika tumekuwa tukijaribu kushauri na kukaa na pande zote mbili kunapokuwa na matatizo yote ya kimikataba, lakini kubwa ambalo tunalifanya sasa hivi ni kuwaelimisha wasanii na wanamichezo kuhusiana na aina ya mikataba wanayoingia ili kuhakikisha tunapunguza ama kuondoa kabisa migogoro ambayo imekuwa ikitokea ambayo ilikuwa inaweza kuepukika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 363

**Ujenzi wa Barabara ya Kagongwa – Isagahe – Bukene Hadi Nzega**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami Barabara ya Kagongwa – Isagahe – Bukene hadi Nzega?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kagongwa – Isagahe – Bukene ni sehemu ya Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo yenye urefu wa kilometa 114 na Kagongwa – Itobo – Nzega yenye urefu wa kilometa 65. Ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara hizi unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa Serikali imekamilisha ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa moja katika Kijiji cha Uduka kilichopo kati ya Bukene na Itobo katika barabara ya Tabora – Mambali – Bukene – Itobo.

Mheshimiwa Spika, aidha, ujenzi wa Barabara ya Nzega – Itobo – Kagongwa sehemu ya Kagongwa hadi Sojo kilometa 18.3 umeishia hatua ya tabaka la tatu la barabara kupitia Mradi wa Bomba la Mafuta. Serikali itakamilisha ujenzi wa matabaka mengine ya barabara hiyo hadi kufikia kiwango cha lami, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika barabara inayotoka Kolandoto – Munze kwenda Mwangongo, je, ni lini sasa Serikali itaanza ujenzi kwa sababu imekuwa ni muda mrefu?

Swali la pili, kwa kuwa ujenzi wa barabara ya lami unakwenda sambamba na uwekaji wa taa, katika Mji wa Solwa tayari ujenzi wa lami kilometa nne zimeshajengwa. Ni lini Serikali itaweka taa mahali pale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli Kolandoto – Mwangongo kwanza ni *trunk road* ambayo imetengewa fedha na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pia hata kwenye bajeti yetu tumetenga fedha ikiwa ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la taa katika Mji Mdogo wa Solwa ninaomba nitoe maelekezo kwa Meneja wa Mkoa wa Shinyanga kwa sababu tunategemea kununua taa nyingi ambazo ziko kwenye mpango wa kufanya *bulk procurement* na maeneo yote ambayo ni miji mikubwa ya wilaya yalishaainishwa ikiwa ni pamoja na Solwa kwamba itapatiwa taa za barabarani, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona. Ninarejea tena maswali yawe mafupi, mkishauliza marefu tu mkiona nimekata mjue wenzenu waliotangulia wamemaliza muda wenu.

Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ni lini mkandarasi wa Barabara ya Itoni – Lusitu atarejea tena na kuanza ujenzi maana mvua zimekwisha na fedha ameshapata?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nitoe maelekezo tu kwa Meneja wa Mkoa na *TANROADS* makao makuu ameshalipwa hela na hali ya hewa imekuwa nzuri. Wamwelekeze mkandarasi aweze kurudi aendelee na kazi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni lini sasa mkataba wa Barabara ya Mlowo – Kamsamba utasainiwa ili barabara hiyo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kila kitu kimeshakamilika na tunategemea mwanzoni kabisa mwa mwezi wa sita mkataba huo utasainiwa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Suma Ikenda, swali la nyongeza.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini barabara ya kutoka Kiwira – Isangati kutoka Mbalizi kufikia Ileje itaanza kujengwa angalau kwa kuanzia Kiwira mpaka Igogo kwa sababu Igogo kuna hospitali kubwa ambapo wagonjwa hasa wajawazito wanashindwa kuifikia kwa wakati? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli hii barabara kwanza haijafanyiwa usanifu, lakini Mkoa wa Mbeya umeshaleta maombi kuifanyia usanifu hiyo barabara ya kutoka Kiwira – Igogwe hadi Isangati ambayo ninaunganisha barabara ya Mbalizi – Shigamba na Mbeya – Tukuyu – Kyela, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Barabara *VETA* – Busweru hadi Igombe TX yenye kilometa 18.2 ina mwaka wa kumi sasa haijakamilika kujengwa. Ni lini kilometa nne zilizobaki zitakamilishwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge barabara hiyo itakamilishwa na tumeiweka kwenye bajeti hii, cha msingi tu hapa ambacho kinakwamisha ni pale ambapo hakuwi na mtiririko mzuri wa fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tuna imani kwamba

katika mwaka ujao wa fedha tutakamilisha hizo kilometa, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hussein Amar, swali la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya kutoka Kahama kilometa 30 kuanzia Nyanholongo – Bukwimba – Izwinya mpaka Kaluma ni mbovu sana. Ninakuomba Mheshimiwa Waziri umuelekeze Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Geita apeleke mashine akaitengeneze barabara hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, mwelekeze.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba nitumie nafasi hii kumuelekeza Meneja wa Mkoa wa Geita ahakikishe kwamba hiyo barabara inapitika na kipindi cha mvua kimeshaisha. Kwa hiyo, mkandarasi arudi *site,* ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, swali la nyongeza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ni lini barabara inayoanzia *Iringa MR* kuelekea Itunundu ya kilometa tano itaanza kujengwa kwa lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, tunasubiri tu tumlipe mkandarasi *advance* kwa sababu kila kitu kimeshakamilika ili aanze kazi kuzijenga hizo kilometa tano, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rehema Migilla, swali la nyongeza.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, Barabara ya Tabora mpaka Ulyanhulu yenye urefu wa kilometa 79 imeshafanyiwa upembuzi yakinifu. Sasa je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, tukishafanya upembuzi na usanifu wa kina kinachosubiri ni kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaijenga hiyo barabara kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Barabara ya Mkiu – Madaba ipo kwenye ilani ya utekelezaji ya Chama Cha Mapinduzi kwa awamu zaidi ya nne. Ni lini sasa Serikali itajenga barabara hii kutoka Mkiu mpaka Madaba kupitia Kijiji cha Mahanje?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, barabara aliyoitaja tunaitambua kuwa ni barabara muhimu sana kiuchumi ambayo ndiyo ninaenda kwenye madini hayo ya chuma na Serikali kwa kweli licha tu ya kuifanyia usanifu lakini tunatafuta chanzo cha uhakika ili barabara hiyo iweze kujengwa tukiwa tunasubiri kuanza mradi huo mkubwa wa uchimbaji wa madini, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana. Aah Mheshimiwa wakati wenzio wanasimama wewe ulikuwa umeketi. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri kashaondoka. Kwa hiyo, basi hadi wakati mwingine. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Ninaleta matangazo tuliyonayo hapa Bungeni leo.

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na tangazo la wageni; tuaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika, tunao wageni 23

wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax ambaye ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na tutaanza na Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe ambaye ni Katibu Mkuu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Jenerali Jacob John Mkunda ambaye ni Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Luteni Jenerali Salum Haji Othman, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Rajab Nduku Mabele ambaye ni Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Jenerali Mstaafu Robert Phillemon Mboma, Mkuu wa Majeshi wa Tano, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Jenerali Mstaafu George Mwita Waitara ambaye ni Mkuu wa Majeshi wa Sita, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia yupo Luteni Jenerali Mstaafu Abdulrahaman Amir Shimbo, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi wa Nane, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Fadhil Omary Nondo, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Shaban Baraghashi Mani, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Rear Admiral Ameir Ramadhan Hassan, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Wanamaji, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Meja Jenerali Iddi Saidi Nkambi, Mkuu wa Kamandi ya Vikosi chini ya Makao Makuu ya Jeshi, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Erick Thomas Mlelwa, Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Akiba, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Obedi Sayore, Kamishna wa Sera na Mipango, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Balozi Wilbert Augustin Ibuge, ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Ulinzi *(NDC)*, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia yupo Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee ambaye ni Mkuu wa Chuo cha *High Command Training Wing*, karibu na ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali Jackon Jairos Mwaseba, Mkuu wa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi, Monduli *(TMA),* karibu sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax anao wageni wengine; kwanza, ni viongozi wa dini kutoka Parokia ya Magu, wakiongozwa na Baba Paroko, Onesmo Shingelwa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Sheikh wa Wilaya ya Magu, Ndugu Nuhu Zahidi, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Musa Juma Issa, Meneja Utawala *Petra Elderly Centre*, karibu sana. *(Makofi)*

Pia wapo ndugu zake kutoka Wilaya ya Magu, wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia wapo familia ya Mheshimiwa Dkt. Tax kutoka Jijini Dar es Salaam, yupo Dkt. Gratian Bamwenda ambaye ni mume wa Mheshimiwa Waziri, karibu sana. *(Makofi)*

Yuo pia Ndugu Agapius Tax ambaye ni mdogo wa Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunao wageni wenu, wapo wageni sita wa Mheshimiwa Balozi Dkt. Pindi Hazara Chana ambaye ni Waziri wa Maliasili na Utalii, hawa ni Madiwani kutoka Mkoa wa Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Abeid Ramadhan Ighondo ambao ni Sheikh wa Mkoa wa Singida na Katibu wa BAKWATA Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ambao ni wasanii wa muziki wa Bongo Fleva kutoka Ludewa Mkoani Njombe, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, kutoka Kata ya Nyatwali, Jimbo la Bunda Mjini wakiongozwa na Mheshimiwa Mawazo Mashimo, Diwani Kata ya Nyatwali, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 31 wa Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, ambao wanafunzi wa Chuo cha St. Bakita kutoka Namanyere, Wilaya ya Nkasi, Mkoani Rukwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 11 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma na watumishi wa Mungu kutoka Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wanafunzi 42 na walimu sita wa Shule ya Msingi Andrea Mwaka kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 50 na walimu saba wa Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi JANESA kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni tisa wa Taasisi ya *Makrina Foundation* kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na Tanga, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna mgeni mmoja hapa alikuwa hajatangazwa, yupo Luteni Mstaafu Samwel Ndomba ambaye ni Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Mstaafu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunalo tangazo la Wafanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2025. Mtakumbuka kwamba siku ya Alhamisi tarehe 1 Mei, 2025, ilikuwa ni Maadhimisho ya Siku

ya Wafanyakazi Duniani ambapo Kitaifa ilifanyika Mkoani Singida na mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa kuwa wakati wa sherehe hiyo wafanyakazi bora huwa wanatambuliwa na kupongezwa, leo nimewaleta ndani ya Bunge Wafanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge ambao wamekaa Jukwaa la Spika ili tuwatambue na kuwapongeza.

Waheshimiwa Wabunge, wa kwanza ni *CPA* Layson Mwanjisi ambaye ni Mhasibu Mkuu kutoka Kitengo cha Fedha na Uhasibu, ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Waheshimiwa Wabunge, akiwa bado amesimama huyu ndiye Mfanyakazi Bora wa Ofisi ya Bunge kwa ujumla. Tunakushukuru sana kwa utumishi wako mzuri na tunakutakia kila la kheri katika kuendelea na majukumu haya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba huyu ndiye mfanyakazi bora wa Ofisi ya Bunge kwa ujumla, wapo wengine ambao ni wafanyakazi bora katika mhimili wetu na katika vitengo mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Ndugu Emmanuel Mrema ambaye ni Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi na huyu yuko Ofisi Binafsi ya Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Grace Bidya, huyu ni Katibu wa Ofisi Binafsi ya Naibu Spika ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu. Romanus Kaduma ambaye ni Dereva Mwandamizi, Ofisi Binafsi ya Katibu wa Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa hawa wengine ninafikiri labda kwa ajili ya ugeni wamekosa nafasi hapa ama wamekaa upande gani. Sawa basi nitawasoma wote ili Taarifa Rasmi za Bunge ziwe na majina yao japo siwaoni hapo juu.

Yupo Ndugu Rehema Kimbe, ambaye ni Msaidizi wa Ofisi Mkuu, Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Elizabeth Malogo, Afisa Sheria I, Idara ya Huduma za Sheria, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Joyce Gadosa, Afisa Sheria I, Idara ya Shughuli za Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Asia Msangi, Mwandisi Taarifa Rasmi za Bunge Mkuu I, Idara ya Kamati za Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, yupo Ndugu Brown Mwangoka, Afisa Utafiti Mkuu I, Idara ya Bajeti, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Emmanuel Mpanda, Mkurugenzi Msaidizi, Idara ya Maktaba na Utafiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Mathew Makungu, Dereva, Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Rehema Mgweno, Afisa Ugavi II, Kitengo cha Ununuzi na Ugavi, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Lukindo Choholo, Mpokezi Mkuu I, Kitengo cha Uhusiano wa Kimataifa, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Christopher Comino, Mpiga Chapa Msaidizi Mkuu II, Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Mary Mtoi Afisa Tehama II, Kitengo cha TEHAMA, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Frank Ngonyani, Msaidizi wa Ofisi Mwandamizi Kitengo cha Ulinzi na Usalama, ahsante sana. *(Makofi)*

Pia yupo Mzee M. Sherehe, Msaidizi wa Kumbukumbu I, Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Waziri Kizingiti, Msaidizi wa Ofisi Mkuu, Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Catus Fredrick, Fundi Mitambo Msaidizi Kitengo cha Menejimenti ya Milki, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu napenda kuwapongeza sana wafanyakazi hawa ambao leo wametambuliwa hapa kwa ufanyakazi bora katika Ofisi yetu ya Bunge, lakini nitumie pia fursa hii kumshukuru Katibu wetu wa Bunge kwa usimamizi mzuri wa hawa wote ambao leo tumeweza kuwatambua hapa.

Kwa hiyo, na wewe Katibu wetu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard na wewe tunakupongeza sana kwa kupata wafanyakazi bora, ahsante sana. *(Makofi)*

Watumishi wetu tunawatakia kila la kheri na pia tunaamini hii itawatia ari zaidi ya kufanya kazi kwa bidii zaidi na kuongeza nidhamu, lakini kuwa mfano bora kwa wale wengine ambao hawakupata fursa kipindi hiki tunaamini watatia bidi zaidi ili waweze kukumbukwa safari ijayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lipo tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge na anawakumbusha kwamba leo saa 10.00 jioni tutakutana sote Ukumbi wa Msekwa, Wabunge wote wawepo bila kukosa.

Waheshimiwa Wabunge, upo mwongozo uliombwa na Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole kuhusu maswali yake ya nyongeza katika swali namba 336 kuhusu kutokujibiwa kikamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 16 Mei, 2025 katika Kikao cha Ishirini na Sita cha Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge, Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole aliomba Mwongozo

wa Spika kuhusu majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Godwin Oloyce Mollel, Naibu Waziri wa Afya wakati alipokuwa akijibu maswali ya nyongeza katika swali namba 336 yaliyoulizwa na Mbunge huyo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenisongole aliuliza maswali ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza, sasa nini kauli ya Serikali ya kuzitaka hizi zahanati, vituo vya afya na hospitali ambazo zinatoza akina mama kinyume na sera yetu ya mwaka 2007?

Swali la pili, sasa hivi mama akienda kujifungua anaambiwa alete nyuzi, dripu una *gloves* na hivyo vifaa siyo vyote vinatumika na vikibaki vinabaki kule hospitali. Nini kauli ya Serikali kuhakikisha hilo jambo haliendelei?

Waheshimiwa Wabunge, wakati anatoa majibu ya maswali hayo ya nyongeza, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba Sera ya Afya ya mwaka 2007 inatumika na ndio inatoa mwongozo wa utoaji wa huduma za afya nchini. Hivyo alimtoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge ikiwa ana hofu kwamba sera hiyo haizingatiwi.

Vilevile Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba mahitaji ya fedha za kununua dawa na vifaa tiba ni makubwa ukilinganisha na fedha ambazo zimekuwa zinapitishwa na Bunge. Aidha, alifafanua zaidi kwamba mahitaji ya bajeti ya kununua dawa ni shilingi bilioni 227 na bajeti inayopitishwa na Bunge ni shilingi bilioni 200 kwa ununuzi wa dawa pekee. Kutokana na hali hiyo utoaji wa huduma ya afya bure kwa akina mama wajawazito imekuwa ikikabiliwa na changamoto hiyo ya kifedha.

Waheshimiwa Wabunge, zaidi ya changamoto hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba zipo changamoto zingine zinazokabilia utoaji wa huduma za afya, kwa akina mama wajawazito katika hospitali, vituo vya afya na zahanati. Changamoto hizo zinatokana na upungufu katika usimamizi wa kibajeti na kiutawala kama vile utoaji wa makadirio ya chini ya

uhitaji wa dawa kuliko uhalisia, fedha zinazokasimiwa kununua vifaa kutotumiwa na kushindwa kutumia fedha zilizopo.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu changamoto iliyodokezwa na Mheshimiwa Mwenisongole kwamba wapo baadhi ya akina mama wajawazito wanaotakiwa na hospitali, vituo vya afya na zahanati kupeleka vifaa kwa ajili ya huduma ya uzazi, kama vile nyuzi, dripu na *gloves* au vifaa vingine na vifaa hivyo siyo vyote vinavyotumika na vikibaki vinabaki hospitali. Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza kwamba ingefaa hospitali, kituo cha afya au zahanati husika zijulikane ili kuweza kubaini chanzo cha tatizo na kujua namna ya kutatua.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Mwenisongole alitumia kanuni ya 53 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kueleza kwamba, hajaridhishwa na majibu yaliyotolewa hivyo aliomba Mwongozo wa Spika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo ya Mheshimiwa Mwenisongole nilitoa mwongozo kwamba, nitapitia *Hansard* ili kuona maswali hayo ya nyongeza pamoja na majibu yake ambayo Mheshimiwa Waziri aliyatoa ili kujiridhisha iwapo maswali ya nyongeza yalijibiwa kikamilifu kwa mujibu wa kanuni zetu.

Waheshimiwa Wabunge, nimepitia *Hansard* na nimeona kwamba Mheshimiwa Mwenisongole alitaka kujua iwapo Sera ya Afya ya mwaka 2007 bado inatekelezwa. Vilevile alitaka kupata kauli ya Serikali kuhusu kwa nini akina mama wajawazito wanaotakiwa kupata huduma bila malipo hutakiwa na hospitali vituo vya afya na zahanati kila wanapokwenda kujifungua kwenda na nyuzi, dripu, *gloves* na vifaa hivyo siyo vyote vinatumika na vinabaki huachwa hospitali. Mheshimiwa Mwenisongole alieleza kwamba majibu ya maswali hayo ya nyongeza hayakuwa ya kuridhisha.

Waheshimiwa Wabunge, *Hansard* zinaonesha wakati Mheshimiwa Naibu Waziri akijibu maswali ya nyongeza alimtoa wasiwasi Mheshimiwa Mwenisongole aliyekuwa na hofu kwamba

Sera ya Afya haitumiki. Mheshimiwa Naibu Waziri alifafanua kwamba Sera ya Afya ya mwaka 2007 ipo na ndiyo inayoongoza utoaji wa huduma za afya nchini katika hospitali, vituo vya afya na zahanati.

Waheshimiwa Wabunge, kwa upande mwingine Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa ufafanuzi kuhusu suala la akina mama wajawazito kutakiwa na hospitali, vituo vya afya na zahanati kupeleka nyuzi, dripu za maji na *gloves* tofauti na tamko la sera ya afya na vifaa hivyo kutorejeshwa kwa wahusika mara baada ya matibabu. Mheshimiwa Naibu Waziri, alisema ni vyema hospitali, vituo vya afya na zahanati zinazotoa maelekezo hayo ya kupeleka vifaa na kutorejesha vifaa vinavyobaki zijulikane ili kujua chanzo na namna nzuri ya kuondokana na changamoto hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Naibu Waziri alieleza zaidi kuwa ziko changamoto nyingine mbalimbali ambazo Wizara inapitia katika utekelezaji wa sera ya afya ambayo ni ufinyu wa bajeti, tatizo la uongozi, makadirio ya chini ya mahitaji ya dawa, kutonunua dawa zinazohitajika kwa wakati na kuwa na fedha ambazo hazitumiwi kununua dawa.

Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa mfano wa Hospitali ya Wilaya iliyopo katika jimbo la Mheshimiwa Mwenisongole ambapo walibaini changamoto hizo walipofanya ziara ya pamoja. Hivyo alieleza kwamba hospitali, vituo vya afya na zahanati hizo zikijulikana itakuwa rahisi kujua chanzo cha tatizo na ufumbuzi wake.

Waheshimiwa Wabunge, pia nimepata fursa ya kupitia Sera ya Afya ya mwaka 2007 ambayo pamoja na mambo mengine katika kipengele cha 5.3.4 kinatoa mwongozo wa afya ya mama na mtoto. Katika kipengele hicho sehemu ya (c)(i), (ii) na (iii) sera hiyo inatoa tamko kwamba Serikali itatoa huduma ya afya bila malipo kwa wanawake wajawazito, watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango na watoto wenye umri chini ya miaka mitano. Lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha kwamba miongozo, mikakati na mipango endelevu inakuwepo kwa nia ya kupunguza

vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi pamoja na kuepusha vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano hasa watoto wachanga.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya uchambuzi huo na kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya naamini kwamba si rahisi hospitali, vituo vya afya na zahanati zote hapa nchini kwa ujumla wake kutaka akina mama wajawazito kupeleka nyuzi, dripu za maji na *gloves* wakati wa kujifungua. Hivyo, ni muhimu Serikali kufanyia kazi changamoto katika suala hili ili hospitali, vituo vya afya na zahanati zenye utaratibu wa kudai akina mama wajawazito kupeleka vifaa zijulikane na changamoto zilizopo zibainishwe na kutatuliwa ili kuweza akina mama wajawazito kupata huduma bila malipo jambo ambalo ndio matamanio ya Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ufafanuzi huo mwongozo wangu ni kuwa nimejiridhisha kwamba, majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya yalikuwa yanajitosheleza kama inavyotakiwa na Kanuni ya 53. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, huo ndio mwongozo wangu na sasa tutaendelea na ratiba iliyo mbele yetu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, aje awasilishe hoja ya Wizara yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Pia naomba hotuba yote kama ilivyowasilishwa iingizwe katika *Hansard. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana wakati nchi yetu ikiwa katika hali ya amani, utulivu na usalama.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuchaguliwa kuwa Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar kuwa Mgombea Urais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha imani kubwa waliyonayo wana CCM kwa viongozi hawa, kutokana na uongozi wao mahiri na imara unaozingatia maslahi ya Taifa. Nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono na kuwaamini viongozi hawa kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa CCM kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu ujao. Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi ni mwanadiplomasia na mwanasiasa mkongwe mwenye uzoefu mkubwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi, ndani ya nchi na hata kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa huu ni Mkutano wa mwisho wa Bunge hili kabla ya Uchaguzi Mkuu mwezi Oktoba, 2025 kwa unyenyekevu mkubwa napenda kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge mwezi Septemba, 2021 na kuniteua kuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mara mbili na nikiwa mwanamke wa kwanza katika historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tangu kupata uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni heshima kubwa si kwangu tu bali ni kwa wanawake wote wa Kitanzania na ni dhamana kubwa kwangu ambayo nitaienzi siku zote za maisha yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninamshukuru pia kwa kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika kipindi cha uongozi wake. Nawashukuru sana wote walioniamini, walionipa ushirikiano na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Wanawake tusikubali kukatishwa tamaa na tusikate tamaa, tuoneshe kwamba tunaweza pale tunapopewa nafasi. *(Makofi)*

Pia ninamshukuru kwa kuendelea kuwaamini Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Jenerali Jacob John Mkunda kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuimarisha Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake hususan Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kuhakikisha Taifa letu linaendelea kuwa na amani, ni imara na lenye utulivu na mshikamano.

Vilevile napenda kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Kassim Majaliwa

Majaliwa Mbunge, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao makini na kwa miongozo mbalimbali wanayonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ninayoiongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge, kwa kuliongoza Bunge kwa weledi na viwango vya hali ya juu. *(Makofi)*

Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika pamoja na Waheshimiwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili kwa umakini na weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Mawaziri wenzangu na Naibu Mawaziri, wote kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa, akisaidiwa na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, pamoja na Wajumbe wa Kamati, kwa maoni na ushauri wanaoendelea kutupatia ikiwa ni pamoja na katika maandalizi ya bajeti hii ambayo ninaiwasilisha. Maoni yao na maelekezo yao tumeyazingatia na yametusaidia sana katika kuboresha makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ninayoiwasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na wenzangu waliotangulia kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu na Taifa kwa kuondokewa na Hayati David Cleopa Msuya, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu, Marehemu Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni, na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani, kanda ya Afrika, Marehemu Profesa Philemon Sarungi aliyewahi kutumikia Taifa letu katika nafasi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Waziri wa Ulinzi na JKT, Marehemu Jaji Fredrick Mwita Werema aliyewahi kuwa

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Marehemu Balozi Juma Volter Mwapachu aliyewahi kuwa Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marehemu Bibi Sifael Mushi, mwanamke aliyeshiriki katika tukio la kuchanganya udongo wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar. Napenda kutoa pole kwa familia, ndugu, jamaa na Watanzania wote kwa kuondokewa na viongozi hao.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kutoa pole kwa Amiri Jeshi Mkuu, familia, ndugu na jamaa kufuatia kifo cha Jenerali Mstaafu David Bugozi Musuguri aliyekuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Meja Jenerali Mstaafu Martin Shiminzi Busungu na Meja Jenerali Mstaafu Charles Mang'ela Mbuge aliyewahi kuwa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa na wanajeshi wote waliopoteza maisha wakiwa kwenye misheni za ulinzi wa amani. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa mwezi Oktoba, 2025 kutakuwa na Uchaguzi Mkuu wa kumchagua Rais, Wabunge na Madiwani; na kwa kuzingatia kazi kubwa iliyofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, naomba kutoa rai kwa Watanzania wote kujitokeza na kutimiza wajibu wao wa kikatiba na kuchagua viongozi watakaoendelea kuwaletea maendeleo pamoja na kudumisha ulinzi, amani, utulivu na usalama. Niwatakie kila la kheri wote watakaogombea nafasi hizo.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu; katika mwaka wa fedha 2024/2025, hali ya mipaka ya nchi yetu yenye urefu wa jumla ya kilometa 5,923.41 ambayo inahusisha eneo la nchi kavu, anga na eneo la maji imeendelea kuwa shwari. Mipaka ya nchi kavu ni baina ya Tanzania na Burundi, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Malawi, Msumbiji, Rwanda, Uganda, Zambia na mipaka ya bahari inajumuisha nchi za Comoros na Shelisheli.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika hapakuwa na matukio ya uhasama yaliyoripotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakanazo mbali na changamoto kadhaa za ulinzi na

usalama. Maelezo ya kina kwa kila mpaka yanaonekana katika aya ya 13 – 23 ukurasa wa 7 – 12 wa hotuba ninayoiwasilisha.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kutatua mgogoro uliodumu kwa muda mrefu Mashariki mwa Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Wakuu wa nchi za Jumuiya za Maendeleo wa Kusini mwa Afrika *(SADC)* na nchi Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* wamesisitiza umuhimu wa kutafuta suluhisho la kuduma kupitia njia za majadiliano na kisiasa. Kufuatia msisitizo huu Wakuu wa Nchi za *SADC* walifikia uamuzi wa kuondoa vikosi vya kijeshi vya *SADC* nchini *DRC* ili kupisha michakato ya kisiasa na majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu naomba kutoa taarifa kuwa vikosi vyetu vinaendelea kurejea salama kabisa. Aidha, napenda kulipongeza Jeshi letu la Ulinzi la wa Wananchi wa Tanzania chini ya Mkuu wa Majeshi Jenerali Jacob John Mkunda na wanajeshi wote kwa uhodari, weredi na kazi kubwa walioifanya katika kutekeleza misheni hii na misheni nyingine zote za ulinzi wa amani na kwa uzalendo wao katika ulinzi wa Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa heshima kubwa naomba kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa uongozi wake mahiri katika kusimamia ulinzi na amani akiwa Amiri Jeshi Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini pia Mwenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025; naanza na tathimini ya makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 87,603,000 kutoka katika mafungu yake matatu yafuatayo; Fungu 38 - NGOME shilingi 22,000,000; Fungu 39 - JKT shilingi 64,403,000 na Fungu 57 - Wizara shilingi 1,200,000.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 Wizara imekusanya jumla ya shilingi 178,759,103.08 ikiwa ni sawa na

204.06% na mchanganuo wa maduhuli kwa kila Fungu umeoneshwa katika Jedwali Na. 1 ukurasa wa 17.

Mheshimiwa Spika, upo utofauti mkubwa katika Fungu 57 ambao umetokana na malipo ya deni la ukodishaji wa minara ya simu yakiwa ni malipo ya mara moja, hali hiyo haitarajiwi kujitokeza tena na kuathiri maduhuli yanayofuata.

Mheshimiwa Spika, tathimini ya utekelezaji wa bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 3,326,230,419,000 na kati ya fedha hizo shilingi 3,008,812,907,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 317,417,512,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Fungu 38 - NGOME liliidhinishiwa fedha za matumizi ya kawaida shilingi 2,491,439,934,000 na shughuli za maendeleo shilingi 48,867,636,000; Fungu 39 - JKT matumizi ya kawaida shilingi 490,652,279,000 na shughuli za maendeleo shilingi 8,549,876,000; Fungu 57 - Wizara matumizi ya kawaida shilingi 26,720,694,000 na shughuli za maendeleo shilingi 260,000,000,000. Muhtasari wa mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na. 2, ukurasa wa 19.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizopokelewa kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 ni kama ifuatavyo; hadi kufikia Aprili, 2025 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 2,605,257,552,583.97 ikiwa ni sawa na 78.3% ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi 2,471,841,028,629.64 ikiwa ni sawa na 82.5% ni matumizi ya kawaida na shilingi 133,416,523,954.33 sawa na 42% kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya kiasi hiki Fungu 38 - NGOME limepokea shilingi 2,042,765,184,281.75 sawa na 81.99% kwa matumizi ya kawaida na shilingi 12,363,521,537.7 sawa na 25.5% kwa shughuli za maendeleo; Fungu 39 - JKT limepokea shilingi 407,035,433,833.03 sawa na 82.96% kwa matumizi ya kawaida na maendeleo shilingi 8,549,876,000 sawa na 100% kwa shughuli za maendeleo na Fungu 57 - Wizara limepokea shilingi

22,040,410,514.86 sawa na 82.48% kwa matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo shilingi 112,503,126,416.63 sawa na 43.27%. Muhtasari wa mchanganuo wa mapokezi ya fedha kwa mafungu yote umeainishwa katika Jedwali Na. 3, ukurasa wa 21.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Aprili, 2025 Fungu 57 - Wizara imepokea uhamisho wa fedha kiasi cha shilingi 1,254,538,735,667 kugharamia miradi ya maendeleo na kati ya fedha hizo, shilingi 1,185,270,693,919 zimetolewa kugharamia ununuzi wa zana na vifaa vya medani kwa matumizi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na shilingi 65,268,041,751.06 kugharamia deni la kimkataba na hivyo kufanya jumla ya bajeti ya fedha za maendeleo kuwa shilingi 1,514,538,735,667 kwa Fungu 57.

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea pia uhamisho wa fedha wenye jumla ya shilingi 103,092,029,422.93 kwa Fungu 38 - NGOME kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa zana na vifaa na hivyo kufanya jumla ya fedha za maendeleo kuwa shilingi 151,959,665,422.93 kwa Fungu 38.

Mheshimiwa Spika, vilevile Fungu 38 - NGOME imepokea uhamisho wa fedha wenye jumla ya shilingi 133,668,246,972.06 kwa matumizi mengineyo na hivyo kufanya jumla ya fedha za matumizi mengineyo kuwa shilingi 242,971,255,037.06. Fedha hizo zimetumika kugharamia operesheni maalumu nchini Msumbiji, ununuzi wa mafuta ya zana na vifaa vilivyotumika kwa ajili ya zoezi la medani, maadhimisho ya siku ya kumbukumbu ya mashujaa, malipo ya madeni ya matibabu, ununuzi wa mavazi, pamoja na kugharamia chakula cha Kuruti.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya fedha za kawaida; fedha zilizotolewa kwa matumizi ya kawaida katika mwaka wa fedha 2024/2025 zimetumika kwa shughuli zifuatazo:-

(a) Matunzo ya zana na vifaa vya Jeshi;

(b) Kuratibu na kusimamia mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi kwa maafisa na askari ndani na nje;

(c) Kuwapatia wanajeshi mafunzo ya awali na kuwaendeleza katika taaluma mbalimbali na uongozi;

(d) Kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya awali ya Kijeshi ukakamavu, kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa na stadi za kazi ili kuweza kujitegemea;

(e) Kutoa huduma za afya na tiba kwa maafisa, askari, watumishi wa umma na familia zao, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na wananchi wanaoishi karibu na Vituo vya Afya vya Jeshi;

(f) Kutatua migogoro ya ardhi;

(g) Kushirikiana na mamlaka za kiraia katika uokozi kwenye majanga mbalimbali, na kulinda miradi ya kimkakati;

(h) Kutoa stahili mbalimbali ikiwemo mishahara, malipo ya likizo kwa maafisa, askari na watumishi wa umma na kuwasafirisha wastaafu na mizigo yao;

(i) Kuimarisha utawala bora na;

(j) Kuimarisha ushirikishwaji wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, mafunzo na mazoezi ya kijeshi; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi na Wananchi wa Tanzania imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi ndani na nje na mafunzo ya awali na ya kuwaendeleza wanajeshi katika taaluma mbalimbali za uongozi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Jeshi lilifanya zoezi la kijeshi la kutimiza miaka 60 ya Jeshi, zoezi la Amani Umoja na kwa kushirikiana na Jeshi la China na mazoezi mawili kwa kushirikiana na Jeshi la Marekani na kuzialika nchi 18 ikiwemo Comoros, Djibouti, Georgia, Kenya, Madagascar, Malawi, Marekani, Mauritius, Morocco, Msumbiji, Shelisheli, Somalia, Ufaransa na Ubelgiji.

Mheshimiwa Spika, aidha Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kupitia Kamandi ya Jeshi la Wanamaji lilifanya zoezi la pamoja na Jeshi la Wananchi kutoka Jamhuri ya India liitwalo *Africa India Key Maritime Engagement*. Zoezi hili lilishirikisha pia nchi nyingine tisa za Afrika ambazo ni Afrika Kusini, Comoros, Djibouti, Kenya, Mauritius, Madagascar, Msumbiji, Shelisheli na Uganda. Mazoezi haya yamechangia katika kuimarisha na kuwajengea uwezo maafisa na askari wake, lakini pia kukuza diplomasia ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa mazoezi na mafunzo haya, pamoja na mambo mengine hutegemea maeneo maalumu yaliyotengwa kwa mazoezi husika. Naomba kupitia Bunge lako Tukufu kutoa rai kwa wananchi kutovamia maeneo ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi Tanzania, kwani kufanya hivyo ni kuhatarisha maisha yao, lakini pia kuhatarisha usalama wa Taifa na kukwamisha shughuli muhimu za kuliweka tayari jeshi letu kukabiliana na matishio yanayoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda pia kuwashukuru Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini, Mheshimiwa Joseph Anania Tadayo, Mbunge wa Mwanga na Mheshimiwa Antipas Zeno Mngungusi, Mbunge wa Malinyi kwa uzalendo wao wa hali ya juu na kuwezesha upatikanaji wa maeneo katika Majimbo yao kwa ajili ya shughuli za Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hususani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na JKT, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kupitia Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matengenezo na matunzo ya zana na mitambo; katika kipindi husika Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kufanya matengenezo na matunzo ya zana na vifaa mbalimbali ili kuliimarisha Jeshi ikiwemo matengenezo na matunzo ya ndege vita na helkopta, matengenezo na maboresho ya *radar,* matengenezo ya magari ya deraya, na silaha mbalimbali, maboresho ya magati na vyelezo, matengenezo ya meli na boti. Vilevile ukarabati wa mitambo na mashine umefanyika katika mashirika ya Mzinga na Nyumbu *(TATC)*.

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imewapatia vijana wa Kitanzania mafunzo kwa mujibu wa sheria na kwa kujitolea katika kambi mbalimbali za JKT. Mafunzo yao yametolewa kupitia Operesheni Miaka 60 ya Muungano ambapo jumla ya vijana 34,000 wa mujibu wa sheria walipatiwa mafunzo wavulana wakiwa ni 24,880 na wasichana ni 9,120 na vilevile yametolewa kwa vijana wa kujitolea kupitia Operesheni Miaka 60 ya Muungano ambapo jumla ya vijana 12,000 wamepatiwa mafunzo, kati yao wavulana ni 8,433 na wasichana ni 3,567.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha wahitimu wote wa kidato cha sita wanapata fursa ya kujiunga na mafunzo ya JKT, miundombinu ya makambi imeendelea kuboreshwa ambapo hadi mwaka huu 2025 JKT imefikia uwezo wa kuchukua vijana 60,000 ikilinganishwa na uwezo wa kuchukua vijana 40,000 mwaka 2021; hili ni fanikio kubwa Mheshimiwa Spika vijana 20,000 kati ya 60,000 ni 30% ambayo tumeweza kuipata ndani ya miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Aidha, mpango uliopo ni kuendelea kuboresha miundombinu na kufungua makambi mpya ili kulipa Jeshi la Kujenga Taifa uwezo wa kuchukua vijana 120,000 ifikapo mwaka 2031 na hivyo kuwezesha wahitimu wote wa kidato cha sita kupata fursa ya kujiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu pamoja na umma wa Watanzania kwamba mafunzo haya yameendelea kuwajengea uzalendo, ukakamavu, umoja wa kitaifa, kuwapatia stadi za kazi na maisha katika nyanja mbalimbali ili wakimaliza mafunzo yao waweze kurejea katika jamii wakiwa raia wema, wakiwa wazalendo, wakiwa wenye uhodari na wenye uwezo wa kujitegemea na kulilinda Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe rai kwa vijana wote wanaopata fursa ya kupata mafunzo haya, kuwa tayari kulitumikia Taifa lao

na kuzitumia stadi walizozipata kwa kujiajiri na kujitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kulitaarifu Bunge Tukufu kuwa kulingana na kifungu cha 3(2)(b) cha Sheria ya Jeshi la Kujenga Taifa, Sura ya 193, Toleo la Urekebu la mwaka 2002; JKT inatakiwa kutoa mafunzo kwa vijana ili kuwawezesha kuwa na sifa za kuandikishwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Aidha, kifungu cha 29(1) cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa, Sura ya 192, Toleo la Urekebu la mwaka 2002 kinaainisha sifa za kuandikishwa katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ambazo ni: -

(i) Awe raia wa Tanzania;
(ii) Awe na tabia na mwenendo mzuri;
(iii) Awe na umri usiopungua miaka 18;
(iv) Awe na akili timamu; na pia
(v) Awe amekidhi vigezo vitakavyowekwa na Mkuu wa Majeshi kadiri atakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, kulingana na kifungu cha 148(2) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania hupokea amri kutoka kwa Amiri Jeshi Mkuu na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 5 cha Sheria ya Ulinzi wa Taifa kimeainisha maeneo ambayo Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa amekasimiwa mamlaka na Amiri Jeshi Mkuu.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania hapo tarehe 01 Septemba, 1964 limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa umakini mkubwa, hata pale palipotokea matishio, matishio hayo yaliweza kudhibitiwa kwa wakati na ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu natoa shukrani za dhati kwa Bunge, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kuendelea kuliamini na kulipa ushirikiano Jeshi letu. *(Makofi)*

Aidha, kwa kutambua kuwa Jeshi la Ulinzi wa Tanzania ni chombo mahsusi kwa shughuli mahsusi ambazo zinahitaji weledi, umakini na uzalendo wa hali juu, nitoe rai kwetu sote kuendelea kuliamini, kulipa uhuru wa kutekeleza majukumu yake bila kuingiliwa kwa kufuata matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Ulinzi wa Taifa na kanuni zake pamoja na sheria nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mara nyingi nimekuwa nikisema Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ni chombo mahsusi kwa shughuli mahsusi, pengine nakuwa sitoi ufafanuzi. Naomba nieleze kidogo, wanajeshi huandikishwa na hawaajiri na mwanajeshi anapoandikishwa anakula kiapo, anakula kiapo kuilinda mipaka ya nchi, anakula kiapo kulinda mamlaka, anakula kiapo kulinda uhuru na anakula kiapo kulinda Katiba na hata Mapinduzi matukufu ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huu, uandikishwaji wa vijana katika Jeshi unatakiwa ufanyike kwa umakini wa hali ya juu na bila kuingiliwa na chombo chochote isipokuwa kufuata matakwa ya Katiba na sheria iliyoweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha kimkakati; Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kilimo unaolenga kuongeza uzalishaji na kujitosheleza kwa chakula kwa vijana na kuipunguzia Serikali gharama ya kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na kuchangia katika usalama wa chakula wa Taifa. Katika msimu wa kilimo 2023/2024 kiasi cha tani 3,222 za mahindi na tani 1,002 za mpunga zilizalishwa. Kati ya kiasi hicho, tani 1,660 za mahindi na tani 1,002 za mpunga zimetumika kulisha vijana wanaohudhuria mafunzo ya JKT na tani 1,542 za mahindi zilizosalia zimechangia katika usalama wa chakula nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara kupitia JKT imeendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania katika uendelezaji wa teknolojia na utafiti wa kilimo na uzalishaji wa miche ya michikichi ya kahawa, mbegu za mpunga na alizeti. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 zimezalishwa tani 96

za mbegu za mpunga na tani 94 za mbegu za alizeti kwa ajili ya matumizi ya ndani na ziada kuuzwa kwa wananchi kwa bei nafuu. Matumizi ya ndani maana yake ni ndani ya JKT.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya Jeshi la Akiba; Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba katika mikoa yote ya Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya wananchi 14,803 walihitimu mafunzo hayo, wanaume wakiwa ni 12,203 na wanawake ni 2,600. Lengo la mafunzo hayo ni kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa ulinzi na kuwajengea uwezo wahitimu kulilinda na kulitumikia Taifa lao. Niwapongeze wahitimu wote na kuwataka waendelee kuviishi viapo vyao vya kulinda raia, kutetea uhuru na uchumi wa nchi na kutii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafunzo haya yamefanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali Mitaa na timu yake nzima kwa ushirikiano wanaotupatia katika kutekeleza jukumu hili muhimu sana. Niwaombe kwa dhati kabisa waendelee kutoa kipaumbele katika kutenga bajeti ili kuwezesha mafunzo haya muhimu kwa Taifa letu kufanyika. Wizara ya Ulinzi kupitia vyombo vyake hutoa mafunzo, lakini mafunzo haya hutakiwa kugharamiwa na bajeti iliyotengwa na TAMISEMI. Kwa hiyo, niwaombe tuendelee kutoa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Maadhimisho ya Miaka 60 ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania; tarehe 01 Septemba, 2024 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania liliadhimisha miaka 60 tangu lilipoasisiwa. Katika kipindi hiki cha miaka 60 kumekuwa na mafanikio makubwa sana ikiwa ni pamoja na kulinda Katiba, Muungano, Mipaka na Uhuru wa Taifa letu. Kupitia Bunge lako Tukufu nitoe pongezi kwa wanajeshi wote kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya kwa weledi, uhodari, kujituma na uzalendo wao wa hali ya juu, wanajeshi wote waliotumikia jeshi letu kwa hii miaka 60 na viongozi wao. Taifa letu ni salama kabisa, ni imara na sisi wote ni mashahidi wa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano na mamlaka za kiraia; Wizara imeendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika shughuli mbalimbali zikiwemo kutoa misaada wakati wa majanga na maafa ambapo kwa mwaka 2024/2025 Wizara ilishiriki katika uokoaji huko Kariakoo, Dar es Salaam kufuatia kuporomoka kwa jengo; uokoaji wakati wa mafuriko Rufiji na Morogoro, na uokoaji wakati wa maporomoko ya matope huko Hanang. Aidha, Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushiriki katika ulinzi wa miradi ya kimkakati na maelezo ya kina yanaoneshwa katika aya ya 45, ukurasa wa 35 – 36. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu utatuzi wa migogoro; kupitia Mpango wa Wizara wa Kutatua Migogoro, Wizara imeendelea kutatua migogoro ya ardhi ambapo migogoro yote inayojulikana imetatuliwa kwa kuhuisha mipaka, kupima maeneo, kufanya uthamini na kulipa fidia katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kiasi cha shilingi 15,349,759,858 zimelipwa kama fidia kwa maeneo tisa ya vikosi, vyuo, shule na minara 17 katika mikoa tisa. Taarifa kamili kuhusu maeneo ambayo mipaka imehuishwa, ardhi imepimwa na fidia imelipwa inaoneshwa katika Jedwali Na. 4, ukurasa wa 43 mpaka 45. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inaendelea na taratibu za kulipa fidia katika maeneo ambayo wananchi hawajalipwa, maeneo hayo yanaonekana katika Jedwali Na. 5, ukurasa wa 46.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utunzaji wa mazingira; Wizara imeendelea kuchukua hatua mahsusi ili kutimiza azma ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya utunzaji wa mazingira na matumizi ya nishati safi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara na taasisi zake imeweza kupanda miti mipya katika maeneo yenye ukubwa wa ekari 964.9. Vilevile Wizara imeendelea na utunzaji wa fukwe katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya nishati safi; Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na kambi zake zinazolisha zaidi ya watu 100 matumizi hayo ya nishati yamefikia 92%; Jeshi la

Kujenga Taifa 98%; Shirika la Mzinga 98% na Shirika la Nyumbu 98%. Kama unavyoona tupo takribani 100% kulingana na maelekezo ya Serikali ambapo tumeelekezwa kufikia mwezi wa sita tuwe tumefikia 100%.

Aidha, matumizi ya nishati safi yamekuwa na mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kuokoa kiasi cha shilingi 2,325,000,000,000 na kuokoa muda katika kuandaa chakula na muda huo kutumika katika mafunzo ya vijana, kulinda afya za wapishi. Aidha, matumizi ya nishati safi yamekuwa shamba darasa kwa vijana wa JKT.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu napenda nitoe shukrani kwa ushirikiano mkubwa tunaoupata kutoka Wakala wa Misitu Tanzania, Wakala wa Nishati Vijijini katika kuisaidia Wizara kutekeleza shughuli za utunzaji wa mazingira na kipekee nitoe shukrani na pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono yake mapana na kusimamia kwa dhati ajenda ya nishati safi ambayo imekuwa na mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za matumizi ya maendeleo; kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara imeweza kutumia fedha za maendeleo ambazo nimekwishazieleza na kuzitaja kwa kutekeleza yafuatayo; nimemaliza kutekeleza yaliyofanywa kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida kwa matumizi ya maendeleo yaliyofanyika ni: -

(a) Kugharamia malipo ya mikataba mbalimbali ya ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya Jeshi. Katika kutekeleza jukumu hili, Wizara imezingatia ushauri uliotolewa na Bunge lako Tukufu, wakati nikiwasilisha hotuba mwaka jana kwamba twende na mahitaji ya teknolojia ya kisasa na kuimarisha utafiti. Tunashukuru sana kwa ushauri huo na tumeuzingatia.

(b) Kugharamia mikataba ya mafunzo na matengenezo ya ndege vita na *helcopters,* pamoja na mafunzo ya marubani;

(c) Kugharamia utafiti na uhuishaji wa silaha, zana na vifaa jeshini;

(d) Kugharamia uboreshaji wa minara ya Mfumo wa Mawasiliano;

(e) Kuendelea kujenga miundombinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na maghala, Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, Ujenzi wa Hospitali Kuu ya Rufaa ya Jeshi Msalato – Dodoma, makazi ya washiriki wa kozi Chuo cha Taifa cha Ulinzi, Bweni la Askari Kapera Wanawake Monduli, Makao Makuu ya Kamandi ya Jeshi, Makazi ya Maafisa na Askari na Shule ya Polisi Jeshi;

(f) Kugharamia ununuzi wa mazao ya msingi;

(g) Kugharamia shughuli za utafiti wa viwanda vya kijeshi kupitia Shirika la Nyumbu na Mzinga;

(h) Ujenzi wa mahanga ya vijana katika kambi mbalimbali za JKT na viteule; na

(i) Kugharamia shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya miradi.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumbu *(Tanzania Automotive Technology Centre);* katika kipindi husika Shirika la Nyumbu limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama yalivyoainishwa katika aya ya 62, ukurasa wa 55.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango wa *TATC* wa miaka 10 wa kuliimarisha Shirika kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Shirika liliidhinishiwa kiasi cha shilingi 15,575,000,000. Hadi kufikia Aprili, 2025 Shirika limepokea jumla ya shilingi 5,000,000,000 ikiwa ni sawa na 32% ya kiasi kilichoidhinishwa. Fedha hizo zimetumika kuanzisha karakana kuu ya kukalibu chuma kwa ajili ya kuzalisha vipuri vya magari, zana za kilimo na za viwandani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza viwanda vya kijeshi Shirika la Nyumbu limekamilisha taratibu za kuingia ubia kwa ajili ya

kuanzisha kiwanda cha kuunganisha magari na kampuni ya *STREIT Group* kutoka Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu. Ubia huu ni wa aina yake ambapo kwa mara ya kwanza viwanda vya kijeshi vinakuwa na ubia na sekta binafsi nchini Tanzania, huu ni utaratibu unaotumika katika nchi zilizoendelea katika viwanda vya kijeshi na hauwezi kuepukika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia imeandikwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu. Manufaa yatakayopatikana kutokana na ubia huu wa kimkakati ni kuongeza mtaji, kuongeza ajira, kupata teknolojia na kuimarisha uwezo wa kuunda magari ya Deraya na kiraia kwa matumizi ya ndani na kuuza nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Mzinga; limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi kama ilivyoainishwa katika aya 66 ukurasa wa 58 na katika mwaka wa fedha Shirika liliidhinishiwa kiasi cha shilingi 6,000,000,000 ambapo hadi kufikia Aprili, 2025 Shirika limepokea shilingi 2,000,000,000 sawa na 33.33% kwa ajili ya ununuzi wa zana na mashine zitakazotumika katika uzalishaji wa mazao ya msingi.

Mheshimiwa Spika, ili kujiimarisha katika viwanda vya kijeshi Wizara kupitia Shirika la Mzinga imeendelea na maandalizi ya kuanzisha kiwanda kipya cha uzalishaji wa mazao ya msingi Mzinga II. Utekelezaji wake utawezesha Shirika kutumia teknolojia ya kisasa na hivyo kuongeza ufanisi na upatikanaji wa uhakika wa mazao ya msingi kwa matumizi ya ndani na ziada kuuzwa nje na kuongeza mapato ya Shirika ya Serikali na kuchangia katika upatikanaji wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Shirika la Uzalishaji Mali (SUMAJKT); limeendelea kuchangia gharama za kuendesha shughuli za malezi ya vijana ikiwa ni pamoja na kukarabati miundombinu, kutoa mitambo katika Skimu za Umwagiliaji wa Kilimo cha Mkakati na kutoa mafunzo ya vitendo. Mwaka wa fedha 2025/2026 Shirika limepanga kujenga mabweni kumi na nne yenye uwezo wa kuchukua vijana 1,120 ambayo yatagharimu jumla ya shilingi 1,242,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika limeendelea na shughuli za kiuchumi katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sekta za ujenzi, viwanda, kilimo, ufugaji, uvuvi, biashara na huduma na ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Shirika limetoa gawio la shilingi 1,034,550,000 kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali (HAZINA). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shirika pia limeimarisha ulinzi wa kimkakati kupitia kampuni yake tanzu ya ulinzi ya *SUMAJKT Guard* ambapo hadi sasa limeanza kutoa huduma ya ulinzi katika vituo vya Treni ya Kisasa *(SGR)* na Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki *(EACOP)* na katika taasisi mbalimbali za Serikali. Miradi ya kimkakati kama hii haina budi kulindwa na taasisi zetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafunzo ya usalama na stratejia; Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Ulinzi - Tanzania imeendelea kutoa mafunzo ya ulinzi, usalama na stratejia kwa maafisa wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na maafisa waandamizi katika utumishi wa umma. Mwaka wa fedha 2024/2025 washiriki 61 wamehudhuria kozi ndefu na washiriki 150 wamehudhuria kozi fupi. Mafunzo hayo yamekuwa na mafanikio makubwa kwa washiriki wa kozi kwa kuwawezesha kupata maarifa juu ya ulinzi na usalama wa Taifa, kisera na kistratejia. Mafunzo haya yanahusisha pia washiriki toka nchi rafiki, na katika kipindi husika mafunzo yametolewa kwa washiriki kutoka Afrika Kusini, Burundi, Eswatini, Ethiopia, India, Kenya, Malawi, Misri, Namibia, Nigeria, Rwanda, Sierra Leone, Uganda, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushirikiano wa kiulinzi kimataifa; Wizara kupitia taasisi zake ikiwa ni pamoja na Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na nchi rafiki katika masuala ya ulinzi katika maeneo mbalimbali ikiwemo mafunzo, mazoezi, misaada ya kitaalamu, zana na vifaa. Vilevile ushirikiano umeimarishwa baina ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Afrika Mashariki katika mafunzo, mazoezi, ubadilishaji wataalamu na operesheni mbalimbali. Nchi hizo ni pamoja na Afrika Kusini, Angola, Algeria, Brazil, Bangladesh, Botswana, Burundi, Canada, Comoros,

Ethiopia, Falme za Kiarabu, Finland, Ghana, Hispania, India, Indonesia, Israel, Jamhuri ya Watu wa China, Jordan, Kenya, Malawi, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Nigeria, Oman, Kuwait, Pakistan, Rwanda, Sri Lanka, Sweden, Ufaransa, Uganda, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi, Zambia na Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupitia Bunge lako Tukufu kutoa shukrani kwa nchi hizi na washirika hawa wa maendeleo, taasisi na mashirika ya kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaotupatia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushiriki katika ulinzi wa amani; Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kimataifa na Kikanda katika operesheni za ulinzi wa amani. Kwa sasa linaendelea kuwa na vikosi vya ulinzi wa amani katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Lebanon chini ya Misheni za Umoja wa Mataifa. Vilevile Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania imeshiriki katika Misheni ya Amani ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo kupitia Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ambayo nimekwishaeleza kwamba imefikia ukingo wake mwezi Machi.

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania katika Operesheni za Ulinzi wa Amani umeiwezesha nchi yetu kujenga uwezo, kuimarisha diplomasia ya ulinzi na kutimiza matakwa ya Umoja wa Mataifa, Jumuiya za Kikanda ya kushiriki katika ulinzi wa amani kimataifa na kikanda kama tulivyosaini mikataba mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya makubwa niliyoyaeleza katika hotuba hii yametokana na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kuimarisha Wizara ya Ulinzi na taasisi zake na kuimarisha ulinzi na amani ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ushiriki katika michezo; katika mwaka wa fedha 2024 Wizara na taasisi zake imeshiriki michezo mbalimbali ikiwemo SHIMIWI iliyofanyika mwezi Oktoba, 2024; michezo ya Mei Mosi iliyofanyika mwezi Mei 2025; Michezo ya Mashirika ya Umma na Makampuni Binafsi yaliyofanyika mwezi Novemba, 2024. Ninapenda kuwapongeza Shirika la Mzinga kwa kushika nafasi ya pili na kuwa mshindi wa jumla katika michezo mbalimbali. Aidha, ninawapongeza viongozi wa Wizara na wachezaji wote waliowezesha Wizara kushika nafasi ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na JKT imeshiriki vilevile katika michezo mingine ndani na nje ya nchi na katika michezo hii wanamichezo wetu waliweza kupata ushindi na kuliletea Taifa letu medali na heshima kubwa. Ninapenda kutumia fursa hii kuwapongeza washindi wote walioshinda katika michezo hii ikiwa ni pamoja na Sajini Alphonce Simbu aliyepata medaii ya fedha katika mbio maarufu duniani za riadha *(Boston Marathon);* Koplo Magdalena Shauri aliyepata medaii ya dhahabu katika mashindano ya michezo ya majeshi kwa nchi za Afrika; *Private* Joseph Panga aliyepata medaii ya fedha katika mashindano ya mbio za nyika; *Private* King Lucas Mwajobaga aliyeibuka na ubigwa katika mashindano ya ngumi za kulipwa; *Private* Yusuph Changalawe aliyeiwakilisha Tanzania katika mashindano ya Olimpiki na mshindi wa mashindano ya michezo ya majeshi kwa nchi za Afrika na timu ya *JKT Queens* iliyoibuka na ubingwa katika Mashindano ya Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati *(CECAFA)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawapongeza Brigedia Jenerali Hassan Rashid Mabena kwa kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano ya *AFCON* yanayotarajiwa kufanyika hapa nchini mwaka 2027 na Meja Mohamedi Haruna Kasui aliyechaguliwa kuwa Rais wa Kamati ya Ufundi wa Mpira wa Kikapu wa Baraza la Michezo ya Majeshi ya Dunia na kuwa Mtanzania na Mwafrika wa kwanza kushika nafasi hiyo tangu mwaka 1948 Baraza hili lilipoanzishwa. Ni heshima kubwa na ni matokeo ya kazi ya diplomasia inayofanywa na Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya makusanyo ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 27,603,000 kutoka mafungu yake matatu; NGOME shilingi 22,000,000; JKT shilingi 64,403,000 na Wizara shilingi 1,200,000 na taarifa ya kina inaonekana katika Jedwali Na. 6, ukurasa wa 69.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya kawaida na maendeleo; katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali inatarajia kutenga jumla ya shilingi 3,645,912,947,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 3,327,115,385,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 318,797,562,000 ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Naomba kurudia.

Mheshimiwa Spika, Fungu 38 – NGOME inatarajiwa kutengewa shilingi 2,733,729,204,000 kwa matumizi ya kawaida na shilingi 48,867,636,000 kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Fungu 39 – JKT inatarajia kutengewa shilingi 567,023,845,000 matumizi ya kawaida na shilingi 9,929,926,000. Fungu 57 – Wizara inatarajia kutengewa shilingi 26,362,336,000 kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 260 kwa shughuli za maendeleeo. Mchanganuo unaoneshwa katika Jedwali Na. 7 ambalo lipo ukurasa wa 70.

Mheshimiwa Spika, shughuli zinazokusudiwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 zitazingatia maeneo ya kipaumbele yafuatayo: -

(i) Kwanza kuendelea kuliimarisha Jeshi kwa zana, vifaa vya kisasa, na rasilimali watu;

(ii) Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi ikiwemo stahili, makazi, mafunzo, matengenezo ya vifaa, na huduma bora za afya;

(iii) Kuendelea kuimarisha miundombinu katika kambi, vikosi, na shule za Jeshi; *(Makofi)*

(iv) Kuendelea kuimarisha uwezo wa Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuboresha miundombinu ili liweze kuchukua vijana wengi zaidi;

(v) Kuendelea kuimarisha Jeshi la Akiba;

(vi) Kuendelea kulinda miradi ya kimkakati kwa maslahi mapana ya Taifa, na kushirikiana na mamlaka za kiraia kadri inavyohitajika;

(vii) Kuimarisha mashirika na taasisi za utafiti wa masuala ya kijeshi;

(viii) Kuimarisha viwanda vya Kijeshi na kuanzisha viwanda vipya kwa kushirikiana na sekta binafsi;

(ix) Kuimarisha ushirikiano na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kikanda na nchi mbalimbali na hivyo kuimarisha diplomasia ya ulinzi;

(x) Kuendelea kutoa mafunzo ya uiinzi na stratejia; na

(xi) Kuendelea kuimarisha mafunzo ya utawala bora na huduma kwa watumishi.

Mheshimiwa Spika, shukrani; kabla sijahitimisha hotuba yangu, ninapenda kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wa Wizara na taasisi zake kwa ushirikiano wanaonipatia, kazi kubwa wanayoifanya na michango yao madhubuti iliyowezesha kutekeleza mpango wa bajeti wa mwaka 2024/2025 kwa mafanikio na maandalizi ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ninayowasilisha.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe - Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga

Taifa, Jenerali Jacob John Mkunda - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Luteni Jenerali Salum Haji Othman - Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Meja Jenerali Rajabu Nduku Mabele - Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Wakuu wa Kamandi wote, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Idara na Vitengo, Wakuu wa Matawi, Wakuu wa Vyuo, Shule na Vikosi vya Jeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ninawashukuru maafisa, askari na watumishi wa umma wote kwa ushirikiano wanaonipatia. Mafanikio tuliyopata ni kutokana na bidii, nidhamu na kujituma kwao. Mwenyezi Mungu awabariki na muendelee kulilinda Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kulishukuru Bunge lako Tukufu, Wizara, taasisi zote na wananchi wote, kwa ushirikiano wanaotoa kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zake katika ulinzi wa nchi yetu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninapenda kuishukuru familia yangu kwa uvumilivu na upendo wao mkubwa unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu na kwa kujiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia, ninawashukuru sana viongozi wa dini kwa kuendelea kuliombea Taifa letu, kumwombea Rais wetu, kuwaombea viongozi wetu mbalimbali. Si kawaida muumini kuwaombea viongozi wa dini, lakini ninaomba na mimi niwaombee viongozi wetu wa dini mwendelee kuwa na afya njema na mwendelee kuimarisha amani na mshikamano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee ninamshukuru Baba Paroko Boniventura Kamuli, Baba Paroko Andreas Buhembo, Baba Paroko Onesmo Shingelwa na Sheikh Nuhu Zahidi Hamis, hawa wote ni kutoka Wilaya ya Magu, Mkoa wa Mwanza kwa kuwa na mimi siku ya leo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee na kwa heshima ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuniamini na kuniteua katika nafasi hii adhimu na kwa uongozi wake mahiri, maono yake mapana na kwa kuhakikisha kuwa Wizara na taasisi zake tunaweza kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi, nchi yetu inaendelea kuwa imara na yenye amani na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukushukuru wewe binafsi, Mawaziri wenzangu na Wabunge wote kwa kunisikiliza. Ninawatakia nyote mafanikio katika Uchaguzi Mkuu na ninaendelea kutoa wito kwa Watanzania wote kujitokeza na kutumia haki yao ya Kikatiba kushiriki ipasavyo katika Uchaguzi Mkuu wa kuchagua viongozi sahihi watakaoendelea kudumisha amani, utulivu na kuliletea maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kazi kubwa iliyofanywa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni dhahiri kuwa kila mmoja wetu anayo sababu ya kumpa sababu ya kuendelea kuliongoza Taifa letu na kuliletea maendeleo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Ulinzi na JKT ambayo ni *www.modans.go.tz.*

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha; kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na taasisi zilizo chini yake inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 3,645,912,947,000; kati ya fedha hizo shilingi 3,327,115,385,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 318,797,562,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeieo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri ahsante sana.

Sasa kama ilivyoada ninamwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na kwa niaba yake Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji anakuja kuwasilisha mawazo ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote ninaomba Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi, na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 iingie yote kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa mapema leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya jumla; kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa taarifa; msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa kifungu cha 6(3) na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Kanuni ya 8 ya Kanuni za Bunge, pamoja na masharti ya Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Bunge kuwa kabla ya taarifa ya utekelezaji na makadirio ya matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi, na Usalama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika mwezi Machi, 2025 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini

chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117(1) hadi 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, mawanda ya taarifa; kwa madhumuni ya kuweka mawanda ya taarifa hii bayana, ninatangulia kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inajumuisha mafungu matatu ambayo ni Fungu 38 – NGOME , Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa na Fungu 57 – Wizara.

Mheshimiwa Spika, muundo wa taarifa; ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kuishauri vyema Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tano zifuatazo: -

Mheshimiwa Spika, moja, sehemu ya kwanza ni utangulizi. Sehemu hii inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi na muundo wa taarifa.

Mbili, sehemu ya pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge.

Tatu, sehemu ya tatu hadi ya nne zinafanya uchambuzi wa utekelezaji wa mipango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kuchanganua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, nne, sehemu ya tano inaonesha maoni na ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya uchambuzi. Sehemu hii pia inahitimisha kwa shukrani na msimamo wa jumla wa Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo; kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Askari Kapera Wanawake *TMA*

Monduli – Arusha. Maelezo ya kina kuhusu mradi uliokaguliwa ni kama inavyoelezwa katika sehemu ya pili ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025; uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na malengo ya makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa hususan fedha za matumizi mengineyo, na upatikanaji wa fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa mafungu yote matatu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari na Aprili, 2025 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Sehemu hii ya taarifa inahusu uchambuzi wa mambo yafuatayo: -

(i) Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati;

(ii) Ukusanyaji wa maduhuli; na

(iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa kazi na Wizara hii. Ninaomba kuliarifu Bunge lako kuwa taarifa ya mtoa hoja ilionesha kwamba Serikali imezingatia sehemu ya ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi milioni 87.6 kwa mafungu yote

matatu. Kwa mujibu wa maelezo ya Wizara hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa shilingi 148.41, sawa na 169%. Kwa ufupi ninaomba niliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwenendo wa makusanyo kwa mafungu yote matatu kwa Wizara hii unaridhisha. Uchambuzi wa kina kuhusu makusanyo ya maduhuli kwa mafungu yote matatu ni kama ilivyoelezwa katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2024/2025 Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha fedha kilichotolewa hadi kufikia mwezi Aprili, 2025.

Mheshimiwa Spika, vilevile katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti za mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa mafungu haya. Ulinganisho huo unaoneshwa katika Jedwali Na. 2 la taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kupitia uchambuzi huo Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

(i) Hadi kufikia mwezi Aprili, 2025 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu ilipokea shilingi 2.6 sawa na 79% ya fedha zilizoidhinishwa.
(ii) Kati ya fedha zilizopokelewa, Fungu 38 - Ngome limepokea 81% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hilo, Fungu 39 - JKT lilipokea 83% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hilo na Fungu 57 - Wizara lilipokea 47% ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya fungu hilo.

(iii) Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. Mathalani, Bunge

liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 - Ngome ikiwa ni 76% ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni 79% ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia mwezi Aprili, 2025.

(iv) Fungu 39 liliidhinishiwa 15% ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo hadi kufikia Aprili, 2025 ni 16% ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.

(v) Fungu 57 lilitengewa asilimia tisa ya bajeti yote ya Wizara. Hadi kufikia Aprili, 2025 lilikuwa limepokea asilimia tano ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuipa kipaumbele kibajeti Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuhakikisha inapata fedha kwa mafanikio yaliyopangwa, suala ambalo linaboresha ufanisi katika utendaji wa Wizara, linaimarisha ulinzi na usalama wa mipaka ya ardhini, majini, na angani pamoja na ustawi wa shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa bajeti hii ni ya mwisho kwa Kamati, itakuwa sio jambo la kiungwana kutoeleza japo sehemu ndogo ya mafanikio ya utekelezaji wa bajeti kwenye sekta ya ulinzi na usalama wa mipaka kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, ninakiri mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha miaka minne ya kibajeti Kamati imeshuhudia mafanikio makubwa katika sekta ya ulinzi na usalama wa mipaka. Mafanikio hayo pamoja na mambo mengine yametokana na kuongezeka kwa bajeti ya Ulinzi kila mwaka na vilevile Serikali kutoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge, na fedha hizo kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kudhihirisha hilo na wakati mwingine kulingana na mahitaji ya kiulinzi na kiusalama, Serikali imekuwa ikifanya uhamisho wa fedha *(reallocation)* kwa lengo la

kuimarisha ulinzi na kuendana na mazingira halisi ya mahitaji katika kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka, pamoja na kuimarisha utendaji wa Jeshi na Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukweli kuwa mambo mengi katika sekta ya ulinzi na usalama hubaki kuwa sitirifu, kwa uchache sana na pasipo ufafanuzi, naomba nitaje mafanikio ambayo Kamati imeyashuhudia kama ifuatavyo: -

1. Ununuzi wa zana na vifaa vya jeshi vya kisasa;

2. Kugharamia ipasavyo matunzo na zana na vifaa vya kijeshi;

3. Kuimarika kwa ulinzi wa mipaka ikiwemo matumizi ya zana za kiteknolojia mipakani;

4. Kushiriki kikamilifu kwa ufanisi katika shughuli za ulinzi wa amani sehemu mbalimbali duniani;

5. Jeshi kuajiri vijana wetu wengi wa Kitanzania;

6. Kuwapatia vijana hawa wa Kitanzania kila mwaka mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi, ukakamavu pamoja na kuwajengea uzalendo;

7. Kugharamia mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi kwa askari na maafisa katika vyuo vya nje na ndani ya nchi;

8. Kuimarika kwa utafiti wa uwihishaji wa silaha, zana na vifaa vya jeshi;
9. Kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi;

10. Kuboresha rada nchini;

11. Kukamilika kwa ujenzi wa makao makuu ya mfano na ya kisasa ya ulinzi wa Taifa, Ngome mjini Dodoma; *(Makofi)*

12. Kukamilika kwa ujenzi wa hospitali ya kisasa ya Jeshi, yenye hadhi ya nyota nne, Msalato Jijini Dodoma; *(Makofi)*

13. Kuimarika kwa shughuli za uzalishaji mali za JKT;

14. Kukamilika kwa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa mahanga kote nchini, ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Jeshi pamoja na ujenzi na ukarabati wa nyumba za askari na maafisa; *(Makofi)*

15. Kuimarika kwa utendaji wa kazi wa mashirika ya Mzinga na Nyumbu;

16. Kuimarika kwa huduma za afya jeshini; na

17. Kuimarika kwa ushirikiano na nchi nyingine katika maeneo ya kiulinzi na kijeshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wote katika eneo la ulinzi na usalama wa mipaka, Serikali ilitekeleza ipasavyo ushauri na maelekezo ya Kamati. Hivyo basi mafanikio haya ni faraja kwa Kamati kwamba inajivunia kwa kuwa ni sehemu ya mafanikio tajwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niendelee na sehemu ya uchambuzi wa mpango wa bajeti wa mwaka ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026; Mpango wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026; ili kujiridhisha na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na dira na dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita, ikiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia

vifaa vya kisasa na zana bora, kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi ya kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumiaji wa umma, kuwapa vijana wa Kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea. Pia kuendeleza tafiti na uhaulishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya kijeshi na kiraia, kuendelea kutoa mafunzo ya jeshi la akiba na kuimarisha ushirikiano wa nchi nyingine katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatawezesha kufikiwa kwa malengo nane ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango uliowekwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2025/2026; kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu 38, 39 na 57 inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi milioni 87.6, kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika mwaka wa fedha 2024/2025 na 2023/2024. Mchanganuo wa makusanyo unaonekana kati Jedwali Na. 4 na Chati Na. 1 ya taarifa hii. Kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la makusanyo kwa mafungu yote ya Wizara hii ni sawa na lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na mwaka huu wa fedha unaoishia, yaani 2024/2025;

(ii) Fungu 39 - JKT linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha 74%;

(iii) Fungu 38 - Ngome linategemewa katika makusanyo kwa kiasi cha 25%;

(iv) Fungu 57 - Wizara linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha 1.4%; na

(v) Mwenendo wa makusanyo kwa Fungu 39 ni mzuri kwani katika mwaka wa fedha 2023/2024 fungu hili liliweza kufikia lengo la makusanyo. Mwenendo wa makusanyo unaonesha kuwa hata kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 fungu hili limefikia malengo ya makusanyo. Hivyo Kamati inaona ipo haja ya kuongeza lengo la makusanyo kwa fungu hili namba 39.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya Kamati inaamini kuwa wizara imeweka malengo katika mafungu yote matatu kwa kuzingatia uhalisia pamoja na changamoto zilizopo na kwamba lengo lililowekwa litafikiwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa inayoombwa kwa mafungu yote matatu ni shilingi trilioni 3.64 kati ya fedha hizo shilingi trilioni 3.32 sawa na 91.3% ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 318.79 sawa na 8.7% ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, ili kukidhi mantiki ya masharti ya kanuni 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma, vifungu na mafungu yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2024/2025. Katika uchambuzi wake, Kamati ilibaini yafuatayo: -

1. Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezwa kwa shilingi bilioni 319.68 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Tofauti hiyo inaongezeko la 8.8%.

2. Kiasi cha fedha kinachoomba kwa ajili ya miradi ya maendeleo kimeongezeka kwa shilingi bilioni 1.38 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa kati ya mwaka wa fedha 2024/2025.

3. Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo haitakuwa na mantiki iwapo Wizara haitahakikisha kuwa mafungu yote yanakamilisha taratibu za awali za kuomba fedha kwa wakati na kwamba Hazina itatoa fedha zinazohusika kama inavyostahiki.

4. Makadirio ya matumizi ya aina zote kwa Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya ulinzi na usalama pamoja na mipaka ya nchi.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Kamati; kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza Kamati inayo mitazamo na maoni yanayojenga msingi wa ushauri utakaotolewa, naomba kubainisha mitazamo na maoni haya kama ifuatavyo: -

1. Utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo, katika Wizara hii kwa mtiririko uliyopangwa ni jambo linalopaswa kuendelea kupewa kipaumbele wakati wote ili kuendana na malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha kwa ajili hiyo.

2. Madeni yote ya kimkataba na ya watumishi wa Wizara yenye muda mrefu tangu mwaka 2014 yaliyohakikiwa yanapaswa kulipwa.

3. Ujenzi wa hospitali ya kijeshi yenye hadhi ya nyota nne katika eneo la Msalato Jijini Dodoma, ni jambo la kupongezwa kwa kuwa itaongeza viwango vya utoaji wa huduma za afya ikiwemo huduma za kibingwa na kibobezi.

4. Upatikanaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Kijeshi, Msalato Dodoma ni suala linalopaswa kupewa kipaumbele na Serikali ili kuhakikisha hospitali hiyo inaanza kutoa huduma mapema mwaka huu.

5. Kukosekana kwa barabara za kiusalama na za kimkakati katika mipaka ya nchi yetu kwa baadhi ya

maeneo kunachangia na kuleta changamoto kwenye doria mipakani. *(Makofi)*

6. Uendeshaji wa mashirika ya kimkakati ya Mzinga na Nyumbu katika sekta na tasnia ya ulinzi kwa maana ya *defence industry* ni jambo la kupewa kipaumbele katika mipango ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Kamati; kutokana na mitazamo na maoni hapo juu, kamati inashauri yafuatayo: -

1. Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti miradi ya maendeleo ya Wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya Taifa.

2. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itoe fedha zote kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa, ya kimkataba na ya watumishi wa Wizara ambayo yana muda mrefu tangu mwaka 2014.

3. Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Fedha, zishirikiane kimkakati katika kuandaa na kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa barabara za kiusalama mipakani. Kufanya hivyo kutasaidia kuboresha barabara za kiusalama na kuweza kupitika muda wote na hivyo kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu.

4. Wizara ya Ulinzi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha zishirikiane kwa lengo la kuweka mkakati wa pamoja, kuhakikisha fedha zinapatikana za ununuzi wa vifaatiba kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Kijeshi iliyopo Msalato Dodoma, kufanya hivyo kutasaidia hospitali hiyo kuanza kutoa huduma kwa askari, maafisa na wananchi kwa ujumla.

5. Serikali itekeleze kikamilifu mipango ya uendelezaji wa Mashirika ya Nyumbu na Mzinga kwa kuyapa

kipaumbele wa kibajeti, kufanya hivyo kutasaidia katika kuendelea kuimarisha mashirika hayo kimkakati na hivyo kupata tija iliyokusudiwa.

6. Wizara iendelee kutekeleza maoni na mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambavyo hayajatekelezwa hususani katika bajeti ya miaka mitatu iliyopita kuanzia mwaka 2022/2023 hadi mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii, aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii, naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa kamati inapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, ambaye ametoa mchango mkubwa katika kuliboresha Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Wizara kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile Kamati inatoa shukrani zake kwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Stergomena Lawrence Tax, kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya kikanuni ya Kamati. Aidha, Kamati inamshukuru Katibu Mkuu, Dkt. Faraji Mnyepe pamoja na watendaji wote wa wizara kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, niishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa, naliomba Bunge lako Tukufu, liipokee taarifa hii na likubali kuhidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FUNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1 Maelezo ya Jumla**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**1.2 Msingi wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa taarifa hii ni majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) na Kifungu cha 7 (1) (a), cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge pamoja na masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge, kuwa kabla ya taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na JKT,

kujadiliwa Bungeni, zilipaswa kuchambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa uchambuzi huo ulifanyika tarehe 20 Machi, 2025 baada ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa chini ya Wizara hii kama ilivyoelekeza Kanuni ya 117(1) hadi 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuweka bayana mawanda ya Taarifa hii, nitangulie kulikumbusha Bunge hili kuwa Wizara ya Ulinzi na JKT inajumuisha Mafungu Matatu (3) ya Kibajeti yafuatayo:-

(i) Fungu 38 - Ngome;
(ii) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na
(iii) Fungu 57 – Wizara

**1.3 Muundo wa Taarifa**

**Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu tano (5) zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza; ni utangulizi; Sehemu hiyo inatoa maelezo ya jumla kuhusu msingi na muundo wa Taarifa.
(ii) Sehemu ya Pili inafafanua matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo uliofanyika kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge.

(iii) Na sehemu ya Tatu hadi ya nne zinafanya uchambuzi wa Utekelezaji wa mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na kuchanganua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

(iv) Sehemu ya Tano inaonesha Maoni na Ushauri wa Kamati kutokana na matokeo ya Uchambuzi. Sehemu hii pia inahitimisha kwa shukurani na msimamo wa jumla wa Kamati

kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Bweni la Askari Kapera Wanawake TMA Monduli - Arusha.

**Mheshimiwa Spika,** Sehemu ya Taarifa hii inaeleza mambo makuu mawili yafuatayo: -

(i) Muhtasari wa maelezo ya miradi iliyotembelewa na kukaguliwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(ii) Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo la sehemu hii ni kuliwezesha Bunge kufuatilia hali ya utekelezaji na upatikanaji wa fedha ilizo ziidhinisha na kupata mantiki ya uamuzi wake wakati wa kujadili makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

### 2.2 Muhtasari wa Maelezo kuhusu Miradi wa Maendeleo iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia msharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilikagua Mradi wa Ujenzi wa Hosteli za Askari Kapera Wanawake, Chuo cha Jeshi- Monduli, Arusha. Madhumuni ya mradi huo ni kujenga jengo la ghorofa moja litakalojumuisha vyumba 40 vya kulala Askari Kapera Wanawake. Mradi huu unajengwa kwa utaratibu wa *Force Account.*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huo, ulianza tarehe 25 Machi, 2024 na umepangwa kukamilika

Mwezi Juni, 2025. Kiasi cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya mradi huo ni **Shilingi 2,225,000,000.00.** Hadi kufikia Mwezi Machi, 2025, Wizara ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 2,225,000,000.00,** sawa na **asilimia 100** ya fedha iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa taarifa za mradi wakati wa ziara ulionesha mambo yafuatayo:-

(i) Hatua iliyofikiwa katika ujenzi ni asilimia 50 ingawaje fedha zilizopokewa ni asilimia 100;

(ii) Matumizi ya fedha iliyopokewa ilifikia asilimia **asilimia 65** ya bajeti iliyotenga na fedha iliyopokelewa.

(iii) Sehemu ya matumizi ya fedha iliyopokewa ilihusisha masuala ya ununuzi ikiwemo ununuzi wa vifaa;

(iv) Kiasi cha fedha ambazo zimepokelewa lakini hazijatumika ni **Shilingi 785,537,545.44** sawa na **asilimia 35.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, ni wazi kuwa utekelezaji umechukua muda mrefu kuliko ilivyotarajiwa. Hali hiyo iliisukuma Kamati kutaka kufahamu sababu. Maelezo ya Wizara yalionesha kuwa mabadiliko ya usanifu yalichangia kuchelewa kwa kuwa yalisababisha ujenzi usimame kwanza kwa muda wa miezi sita (6).

**Mheshimiwa Spika,** Jambo moja muhimu lililopokelewa vizuri na Kamati, ni ufafanuzi kwamba, pamoja na kuchelewa huko, ifikapo Mwezi Juni, 2025 Mradi utakuwa umekamilika kama ilivyopangwa. Kamati ina maoni kuwa Wizara inapaswa kusimamia ipasavyo mradi huo na kuhakikisha unakamilika mwezi Juni, 2025, lakini kwa kuzingatia thamani ya fedha na viwango vya ujenzi. Ikiwa hivyo, lengo la kuwezesha Askari Kapera Wanawake kupata makazi ya kisasa litafikiwa ipasavyo.

### 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na matokeo ya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ina maoni kuwa, Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ya Wizara hii kutokana na umuhimu wake ambao unatokana na asili ya majukumu ya Wizara. Halikadhalika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za Maendeleo kwa kiwango kinachoridhisha kwa Wizara hii kwani inasaidia kuleta tija na ufanisi kwa Ustawi wa Taifa letu

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo na upatikanaji wa fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, kwa mafungu yote Matatu ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Januari na Aprili, 2025 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Sehemu hii ya taarifa inahusu uchambuzi wa mambo yafuatayo:-

(i) Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati
(ii) Ukusanyaji wa Maduhuli
(iii) Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina

### 3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kuchambua Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilishauri masuala mbalimbali yanayopaswa kufanyiwa kazi na Wizara hii. Naomba kuliarifu Bunge lako kuwa, taarifa ya Mtoa Hoja ilionesha kwamba, Serikali imezingatia sehemu ya ushauri uliotolewa na Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ushauri ambao haujatekelezwa kikamilifu unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**3.3 Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Wizara ilikadiria kukusanya maduhuli yenye jumla ya **Shilingi 87,603,000.00/=** kwa Mafungu yote matatu (3).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa maelezo ya Wizara, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025 kiasi cha fedha za maduhuli kilichokuwa kimekusanywa kilikuwa **Shilingi 148,414,103.08/=** sawa na **asilimia 169** ya lengo la mwaka lililopangwa. Kamati ilibaini kuwa kiasi kilichokusanywa ni ongezeko kwa **Shilingi 121,124,083/=** sawa na **asilimia 210** ikilinganishwa na makusanyo ya kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ambayo yalikuwa **Shilingi 57,635,020.00/=**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa makusanyo hayo yamechangiwa na Mafungu yote matatu ya Wizara ambapo; Fungu 38 (Ngome) limekusanya **asilimia 110** ya lengo lililowekwa na Fungu 39 (JKT) limekusanya **asilimia 100** ya lengo lililowekwa na Fungu 57 (Wizara) limekusanya **asilimia 7,517** ya lengo lililowekwa.

**Mheshimiwa Spika,** ongezeko hilo kwa Mwaka huu wa fedha 2024/2025 kwa Fungu 57 (Wizara) limetokana na malipo ya deni la ukodishaji wa simu. Hali hii ni tofauti na Mwaka wa fedha,

2023/2024 ambapo hadi kufikia Aprili, 2024 Wizara haikuwa imekusanya kiasi chochote cha fedha.


**Mheshimiwa Spika,** vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 na Grafu Na. 01 hapa chini.

**JEDWALI NA 1:** *Mchanganuo wa Makadirio na Makusanyo ya Mapato*

| FUNGU | MAKADIRIO | MAKUSANYO | % YA JUMLA YA MAKUSANYO |
|---|---|---|---|
| 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 24,156,103.08 | 110 |
| 39 - JKT | 64,403,000.00 | 64,403,000.00 | 100 |
| 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 90,200,000.00 | 7,516 |
| **Jumla** | **87,603,000** | **178,759,103** | **204** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***


**GRAFU NA 1:** *Ulinganisho wa lengo na Makusanyo halisi ya Mapato*




***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Makusanyo yaliyopatikana kwa kila Fungu kufikia Mwezi Aprili, 2025 na Makusanyo yaliyopatikana katika kipindi kama hicho katika Mwaka 2023/2024 kama inavyoonekana katika **Grafu na 2** hapa chini: -

***GRAFU NA 2:*** *Ulinganisho wa Makusanyo 2023/2024 na 2024/2025*




***Chanzo: Randama za Wizara 2023/2024 na 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya kufanya Uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa: -

(i) **Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome** hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025 ilikusudiwa kukusanya angalau asilimia 75 ya lengo lililowekwa lakini katika utekelezaji Fungu hilo limekusanya asilimia 110 ya lengo lililowekwa kwa mwaka;

(ii) **Makusanyo ya Fungu 39 – JKT** hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025 ilikusudiwa kukusanya angalau asilimia 75 ya lengo lililowekwa lakini katika utekelezaji Fungu hilo limekusanya asilimia 100 ya lengo lililowekwa kwa mwaka;

(iii) **Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara**, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025 ilikusudiwa kukusanya angalau asilimia 75 ya

lengo lililowekwa lakini katika utekelezaji Fungu hilo limekusanya asilimia 7,516 ya lengo ambalo liliwekwawekwa kwa mwaka;

**Mheshimiwa Spika,** ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa, umeisaidia Kamati kubaini kuwa mwenendo wa makusanyo ni mzuri kwa mafungu yote; kwani Fungu 38 (Ngome) lilikuwa limekusanya asilimia 110 ya lengo lilowekwa kwa mwaka, Fungu 38(JKT) lilikuwa limekusanya asilimia 100 ya lengo lililowekwa na Fungu 57(Wizara) lilikuwa limekusanya asilimia 7,516 ya lengo lililowekwa kwa mwaka.

### 3.4 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya kupokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2024/2025, Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kufanya ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi yote ya Wizara na kiasi cha Fedha kilichotolewa hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekana katika **Jedwali Na. 02** hapa chini.

***JEDWALI NA 2:*** *Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa kwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57*

| Fungu | Fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka 2024/2025 | fedha ya Asilimia zilizoidhinishwa | Fedha zilizopokelewa kufikia Aprili, 2025 | fedha ya Asilimia zilizopokelewa | fedha ya Asilimia zilizopokelewa |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 38 | 2,540,307,570,000.00 | 76 | **2,055,128,705,819.45** | 81 | 79 |
| 39 | 499,202,155,000.00 | 15 | **415,585,309,833.03** | 83 | 16 |
| 57 | 286,720,694,000.00 | 9 | **134,543,536,931.49** | 47 | 5 |
| | **3,326,230,419,000.00** | **100** | **2,605,257,552,583.97** | 79 | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, Kupitia uchambuzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea **Shilingi 2,605,257,552,583.97/=** sawa na **asilimia 79** ya fedha zilizoidhinishwa; na

(ii) Kati ya fedha zilizopokelewa, Fungu 38 (Ngome) limepokea **asilimia 81** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hilo, Fungu 39 (JKT) limepokea **asilimia 83** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Fungu hilo na Fungu 57 (Wizara) limepokea **asilimia 47** ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya fungu hilo;

(iii) Serikali ilizingatia uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii. Mathalani, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 (Ngome) ikiwa ni **asilimia 76** ya Bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni **asilimia 79** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara hadi kufikia Mwezi Aprili, 2025;

(iv) Fungu 39 liliidhinishiwa **asilimia 15** ya bajeti yote ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo hadi kufikia Aprili, 2025 ni **asilimia 16** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara; na

(v) Fungu 57 ilitengewa **asilimia 9** ya bajeti yote ya Wizara, hadi kufikia Aprili, 2025 ilikuwa imepokea **asilimia 5** ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuipa kipaumbele kibajeti Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kuhakikisha inapata fedha kwa mtiririko uliopangwa suala ambalo linaboresha ufanisi katika utendaji wa wizara, linaimarisha ulinzi na usalama wa mipaka ya ardhini, majini na angani pamoja na ustawi wa shughuli za kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa bajeti hii ni ya mwisho kwa Kamati, itakuwa sio jambo la kiungwana kutoeleza mafanikio ya utekelezaji wa Bajeti kwenye Sekta ya Ulinzi na Usalama wa Mipaka kwa kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, nikiri mbele ya Bunge lako tukufu kwamba, katika kipindi cha miaka minne ya kibajeti; Kamati imeshuhudia mafanikio makubwa katika Sekta ya ulinzi na usalama wa wa mipaka. Mafanikio hayo yametokana na kuongezeka kwa Bajeti ya Ulinzi kila mwaka na vilevile Serikali kutoa fedha kama zilivyoidhinishwa na Bunge na fedha hizo kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kudhihirisha hilo, wakati mwingine kulingana na mahitaji ya kiulinzi na usalama; Serikali imekuwa ikifanya uhamisho wa fedha (Reallocation between) kwa lengo la kuimarisha ulinzi na kuendana na mazingira halisi ya mahitaji katika kuimarisha ulinzi na usalama wa mipaka pamoja na kuimarisha utendaji wa Jeshi na Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukweli kuwa mambo mengi katika sekta ya ulinzi na usalama hubakia kuwa sitirifu; kwa uchache na pasipo ufafanuzi, naomba nitaje mafanikio ambayo Kamati imeyashuhudia kama ifuatavyo;-

(i) Ununuzi wa zana na vifaa Jeshi vya kisasa;

(ii) Kugharamia ipasavyo matunzo ya zana na vifaa vya kijeshi;

(iii) Kuimarika kwa ulinzi wa mipaka ikiwemo matumizi ya zana za teknolojia mipakani;

(iv) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za ulinzi wa amani sehemu mbalimbali Duniani;

(v) Jeshi kuajiri vijana wengi wa Kitanzania. Katika kipindi cha miaka minne vijana zaidi ya maelfu wamepata ajira jeshini;
(vi) Kuwapatia vijana wa kitanzania kila mwaka mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi, ukakamavu pamoja na kuwajengea uzalendo;
(vii) Kugharamia mafunzo mbalimbali ya kozi za kijeshi kwa Askari na Maafisa katika vyuo vya nje na ndani ya nchi;
(viii) Kuimarika kwa utafiti wa uhuishaji wa silaha, zana na vifaa jeshi;
(ix) Kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi;
(x) Kuboresha RADAR nchini;
(xi) Kukamilika kwa ujenzi wa Makao Makuu ya mfano na ya Kisasa ya Ulinzi wa Taifa (NGOME) Mjini Dodoma;
(xii) Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali ya kisasa ya Jeshi yenye Hadhi ya Nyota nne, Msalato Jijini Dodoma;
(xiii) Kuimarika kwa shughuli za uzalishaji mali za JKT;
(xiv) Kukamilka kwa miundombinu mbalimbali ikiwemo ujenzi wa mahanga kote nchini, ujenzi na ukarabati wa Hospitali za Jeshi pamoja na ujenzi na ukarabati wa nyumba za Askari na Maafisa;
(xv) Kuimarika kwa utendaji kazi wa Mashirika ya MZINGA na NYUMBU;
(xvi) Kuimarika kwa huduma za afya Jeshini; na
(xvii) Kuimarika kwa uhusiano na ushirikiano na nchi nyingine katika eneo la kijeshi na kiulinzi.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wote, katika eneo la ulinzi na usalama wa mipaka, Serikali ilitekeleza ipasavyo ushauri wa Kamati. Hivyo basi, mafanikio hayo ni faraja kwa Kamati; na kwamba inajivunia kwa kuwa ni sehemu ya mafanikio tajwa.

**Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba niendelee na sehemu ya uchambuzi wa mpango wa Bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA BAJETI NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilipitia majukumu makuu ya Wizara na Kubaini kuwa makadirio ya mapato na matumizi yanayopendekezwa yanalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi wa Wizara katika utekelezaji wa majukumu hayo kulingana na Dira na Dhima ya Wizara.

**Mheshimiwa Spika,** lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu sita likiwemo kuliongezea uwezo wa kimedani Jeshi la ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kulipatia vifaa vya kisasa na zana bora; kuboresha mazingira ya kufanyia kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma, Kuwapa Vijana wa kitanzania mafunzo ya awali ya kijeshi na stadi za kazi ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na uwezo wa kujitegemea, kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa ajili ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa matumizi ya Kijeshi na kiraia, kuendelea kutoa mafunzo ya Jeshi la Akiba na kuimarisha ushirikiano na nchi nyingine katika Nyanja za kijeshi na kiulinzi.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha kufikiwa kwa malengo Nane (8) ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati kwa kuzingatia mpango kazi uliowekwa.

### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026


**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 87,603,000.** Kiasi hiki ni sawa na kiasi kilichopangwa kukusanywa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2023/2024. Mchanganuo wa Makusanyo unaonekana katika **Jedwali Na. 04.** na **Chati Na. 01** hapa chini: -

***JEDWALI NA 3:*** *Mchanganuo wa Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2025/2026*

| **Fungu** | **Makadirio** | **Asilimia ya lengo la Wizara** |
|---|---|---|
| Fungu 38 - Ngome | 22,000,000.00 | 25 |
| Fungu 39 - JKT | 64,403,000.00 | 74 |
| Fungu 57 - Wizara | 1,200,000.00 | 1.3 |
| **JUMLA** | **87,603,000.00** | **100** |

***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

***CHATI 1:*** *Mchanganuo wa asilimia ya Makadirio ya Maduhuli kwa mwaka 2025/2026*




***Chanzo: Randama ya Wizara 2025/2026***

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii ni sawa na lengo la Makusanyo liliowekwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 na mwaka huu wa fedhaunaoishia yaani 2024/2025;
(ii) Fungu 39 (JKT) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 74;**
(iii) Fungu 38 (NGOME) linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha **asilimia 25;** na
(iv) Fungu 57 (Wizara) linategemewa kwa makusanyo kwakiasi cha **asilimia 1.4**
(v) Mwenendo wa makusanyo kwa Fungu 39 ni mzuri kwani katika mwaka wa fedha 2023/2024 Fungu hili liliweza kufikia lengo la makusanyo. Mwenendo wa makusanyo unaonesha kuwa hata kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025 Fungu hili limefikia malengo ya makusanyo. Hivyo Kamati inaona ipo haja ya kuongeza lengo la makusanyo kwa Fungu hili.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaamini kuwa Wizara imeweka malengo katika mafungu yote matatu kwa kuzingatia uhalisia pamoja na changamoto zilizopo na kwamba lengo liliowekwa litafikiwa katika mwaka wa fedha 2025/2026.

### 4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

**Mheshimiwa Spika**, maelezo yaliyotolewa na Wizara mbele ya Kamati yalibainisha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote matatu ni **Shilingi 3,645,912,068,000.00/=.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,327,114,506,000/=** sawa na **asilimia 91.3** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 318,797,562,000.00/=** sawa na **asilimia 8.7** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma *(Items),* Vifungu *(Subvotes)* na Mafungu *(Votes)* yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa

na kutekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

(i) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Shilingi 319,681,649,200/=** ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025. Tofauti hiyo ni ongezeko la **asilimia 8.8**;

(ii) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimeongezeka kwa **Shilingi 1,380,050,000/=** ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2024/2025.

(iii) Kati ya Shilingi **318,797,562,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, **asilimia 15.3** ni kwa ajili ya Fungu 38 - Ngome, **asilimia 3.1** ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na **asilimia 81.5** ni kwa ajili ya Fungu 57 Wizara;

(iv) Ongezeko la fedha za miradi ya maendeleo halitakuwa na mantiki iwapo Wizara haitahakikisha kuwa Mafungu yote yanakamilisha taratibu za awali za kuomba fedha kwa wakati na kwamba HAZINA itatoa fedha zinazohusika kama inavyostahili;

(v) Makadirio ya matumizi ya aina zote katika Wizara hii yamezingatia umuhimu wa kufanikisha uimarishaji wa hali ya ulinzi na usalama pamoja na mipaka ya nchi;

(vi) Makadirio ya matumizi yaliyowasilishwa yasipopitishwa na Bunge kwa kiasi hicho au kwa nyongeza zaidi, Wizara itashindwa kutekeleza majukumu yake na shughuli za kiuchumi pamoja na za umma zitakuwa matatani.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI, USHAURI WA KAMATI NA HITIMISHO

### 5.1 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na uchambuzi kama nilivyoeleza, Kamati inayo mtizamo na maoni yanayojenga msingi wa ushauri utakaotolewa. Naomba kubainisha mtazamo na maoni hayo kama ifuatavyo: -

(i) Utoaji wa fedha za miradi ya maendeleo katika Wizara hii kwa mtiririko uliopangwa ni jambo linapaswa kuendelea kupewa kipaumbele wakati wote ili kuendana na malengo yaliyokusudiwa wakati Bunge linaidhinisha fedha kwa ajili hiyo.
(ii) Madeni yote ya kimkataba na ya watumishi wa Wizara, yenye muda mrefu tangu mwaka 2014 yaliyohakikiwa yanapaswa kulipwa.

(iii) Ujenzi wa Hospitali ya kijeshi yenye Hadhi ya Nyota Nne katika eneo la Msalato Jijini Dodoma ni jambo la kupongezwa kwa kuwa itaongeza wigo wa utoaji huduma za afya ikiwemo huduma za kibingwa na kiubobezi;

(iv) Upatikanaji wa Vifaa Tiba katika Hospitali ya Rufaa ya kijeshi Msalato Dodoma ni suala linalopaswa kupewa kipaumbele na Serikali ili kuhakikisha Hospitali hiyo inanza kutoa huduma mapema mwaka huu;

(v) Kukosekana kwa barabara za kiusalama na za kimkakati katika Mipaka ya nchi yetu kwa baadhi ya maeneo kunachangia changamoto kwenye doria mipakani; na

(vi) Uendelezaji wa Mashirika ya kimkakati ya MZINGA na NYUMBU katika Sekta na tasnia ya ulinzi (Defence industry) ni jambo la kupewa kipaumbele katika mipango ya nchi.

### 5.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na mtazamo na maoni hapo juu, Kamati inashauri yafuatayo: -

(i) Serikali iendelee kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili wa kibajeti miradi ya maendeleo ya Wizara ili kupata tija iliyokusudiwa kwa maslahi mapana ya Taifa.

(ii) Katika Mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali itoe fedha zote kwa ajili ya kulipa madeni yaliyohakikiwa ya kimkataba na ya watumishi wa Wizara ambayo yana muda mrefu tangu mwaka 2014.

(iii) Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa pamoja na Wizara ya Fedha zishirikiane kimkakati katika kuandaa na kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa barabara za kiusalama mipakani. Kufanya hivyo kutasaidia kuboresha barabara za kiusalama kuweza kupitika muda wote na hivyo kuimarisha ulinzi wa mipaka.

(iv) Wizara ya Ulinzi kwa Kushirikana na Wizara ya Afya na Wizara ya Fedha zishirikiane kwa lengo la kuweka mkakati wa pamoja kuhakikisha zinapatikana fedha za ununuzi wa Vifaa Tiba kwa ajili ya Hospitali ya Rufaa ya Kijeshi iliyopo Msalato Dodoma. Kufanya hivyo kutasaidia Hopsitali hiyo kuanza kutoa huduma kwa Askari, maafisa na wananchi kwa ujumla.

(v) Serikali itekeleze kikamilifu Mipango ya Uendelezaji wa Mashirika ya NYUMBU na MZINGA kwa kuyapa kipaumbele kibajeti. Kufanya hivyo kutasaidia katika kuendelea kuimarisha mashirika hayo kimkakati na hivyo kupata tija iliyokusudiwa.

(vi) Wizara iendelee kutekeleza Maoni na Mapendekezo ya Kamati yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali ambayo hayajatekelezwa hususan katika Bajeti za miaka mitatu iliyopita ya 2022/2023 ,2023/2024 na 2024/2025.

### 5.3 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Vita Rashid Kawawa, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Vincent Paul Mbogo, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdi Hija Mkasha, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Ali Juma Mohamed, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Bupe Nelson Mwakang'ata, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Balozi Liberata Mulamula, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Daniel Tlemai Awack, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Alfred James Kimea, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Edwin Enosy Swalle, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fakharia Shomar Khamis, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Felister Deogratius Njau, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Grace Victor Tendega, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Maulid Saleh Ali, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Minza Simon Mjika, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Muharami Shabani Mkenge, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Mwinyikondo Rajab Mustafa, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Maimuna Salum Mtanda, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Zahor Mohammed Haji, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Stagomena Lawrence Tax (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika,** Vilevile, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Idelphonce Leornad, kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge. Aidha, niishukuru Sekretariat ya Kamati kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la

Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono Hoja na naomba kuwasilisha.

Vita Rashid Kawawa, (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**
20 Mei, 2025

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji kwa niaba ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Vita Rashid Kawawa. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuweka askari wa JWTZ Manda, Ludewa. Kule ilikuwa ni mapito ya wageni wengi ambao nia zao zilikuwa hazijulikani. Askari wale wanafanya kazi kubwa na nzuri sana ya kulinda mpaka ule, hivyo naomba wapewe gari, boti kubwa na la kasi na watafutiwe eneo kubwa maeneo ya Lutala ili kianzishwe kikosi kamili cha jeshi Ludewa.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, Waziri wa Ulinzi kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ya ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu. Katika kipindi chake akiwa Waziri wa Ulinzi, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno katika ulinzi na amani na kupelekea kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio makubwa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, bado kuna wapiganaji wetu ambao ni wastaafu na wengine walishiriki kwenye vita kwa kulinda mipaka yetu hususani vita ya Kagera, wanalalamikia stahiki zao kutolipwa kikamilifu. Kwa kuzingatia wamefanya kazi kwa uzalendo mkubwa na iwe motisha kwa askari wetu, napendekeza Serikali iangalie jinsi ya kutatua changamoto hii na

kuangalia upya stahiki zao ikiwemo kuboresha mafao ya pensheni zao.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Wizara ya Ulinzi kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu kuangalia jinsi ya elimu ya ulinzi na usalama kuunganishwa kwenye mitaala ya elimu. Pia Serikali iendelee kuboresha mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa ikiwemo mafunzo ya uzalendo na ujasiriamali. Kutokana na mafaniko makubwa ya mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria, Serikali irudishe utaratibu wa mafunzo hayo kwa miezi kumi na mbili na mafunzo haya yawe maandalizi ya kuwajenga vijana kwenye uzalendo na ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo tutakuwa na mchangiaji mmoja kisha mtoa hoja atakuja ahitimishe hoja yake.

Mheshimiwa Geophrey Mizengo Pinda, mchangiaji wetu. *(Makofi)*

Mtoa Hoja ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi ya kuwa mchangiaji pekee kwenye Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kunipa nafasi ya kuwa mpambe wake leo, lakini kipekee kabisa niishukuru Kamati kwa wasilisho lake na katika mazingira ya kawaida yale yote ambayo yamependekezwa na Kamati yanakwenda kufanyiwa kazi na Wizara ili kuleta ufanisi uliosahihi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sikutarajia kuwa mchangiaji pekee, kwa hiyo wakati mwingine unaishiwa hata maneno ya kupangilia habari, lakini ukweli ni kwamba maeneo ambayo Mheshimiwa Waziri ameyawasilisha hapa katika bajeti yake ni maeneo

muhimu kabisa kabisa na sisi kama Wabunge lazima tukayafanyie kazi kwa usahihi wa kutosha kabisa kwa sababu ni maeneo ya kiushahuri na chombo hiki kwa umuhimu wake kwa kweli katika baadhi ya maeneo ambayo kimsingi yanatakiwa kuzingatiwa ni yale maeneo ambayo tunakwenda kuyatumia kwa shughuli za jeshi.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu ushahuri kwa wananchi katika maeneo haya kimsingi huwa ni maeneo hatarishi kwa sababu matumizi yale ya kijeshi huwa yanabaki yanaacha baadhi ya masalia ya vyombo ambavyo vilitumika huko kama mabomu na nini, kwa hiyo, maeneo yote haya ambayo ni maeneo maalumu kwa ajili ya matumizi ya jeshi nitoe tu wito kwa Watanzania wenzangu kwa kweli tusipende kuyachezea chezea maeneo haya kwa sababu ni maeneo hatarishi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna hiyo niombe tu yale maeneo tuliyoyabainisha kwa ajili ya matumizi ya jeshi wananchi wa kawaida tusipende kwenda kuvamia maeneo haya kwa sababu yamekuwa hayana matokeo mazuri kwa wananchi wengine wanaokota yale masalia ya mabomu, wanayachezea na wakati mwingine yanaleta madhara.

Mheshimiwa Spika, mimi sina maelezo marefu, tumuache mtoa hoja aweze kwenda kuhitimisha jambo lake, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax, uje uhitimishe hoja yako. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ahsanteni Waheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo asubuhi katika Bunge lako Tukufu niliwasilisha hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu makadirio na mapato ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Napenda kukushukuru sana, sana

kwa namna ulivyosimamia na kuongoza kwa umakini wasilisho langu na kumruhusu mchangiaji mmoja aweze kuchangia katika mjadala wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, nipende tu pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, wengine mlinipa maoni hata kabla ya kuchangia, niseme tu kwamba maoni yote mliyonipatia nimeyapokea na tutayafanyia kazi na wale waliotamani kuchangia bado wanaweza wakatupa michango, tutaipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa pia napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Vita Rashid Kawawa, Mbunge wa Namtumbo na Makamu wake Mwenyekiti Mheshimiwa Vincent Paul Mbogo, Mbunge wa Nkasi Kusini na Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni yao na ushauri walioupatia, ushauri umewasilishwa, tumeupokea na ni wahakikishie kama ilivyokawaida tutauzingatia, kama siyo kwa 100%, kwa kiasi kikubwa kadiri itakavyowezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpo hapa kutushauri na kama alivyosema aliyekuwa akiwasilisha Taarifa ya Kamati tunashukuru sana kuona kwamba mmeridhishwa na utekelezaji wa maoni mliyokwisha yatoa na mmeendelea kutupa maoni mengine ambayo tutaendelea kuyafanyia kazi. Tunashukuru kwa uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji kuhusu makadirio na hata sisi wenyewe uchambuzi wenu umetufungua macho zaidi, tutaendelea kufanya kazi kuhakikisha kwamba yale yote mliyoyasema, changamoto mlizoziainisha zinafanyiwa kazi kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ushauri mlioutoa ni pamoja na Serikali kutoa kipaumbele katika uzito wa kibajeti katika miradi ya kimaendeleo na hususani mmesisitiza suala la mtiririko mmetoa ushauri kuhusu kulipa madeni, mmetoa ushauri kuhusu ujenzi wa barabara za kimkakati na kiusalama na kuweka mkakati wa pamoja kama Serikali kuhakikisha kwamba ujenzi wa Hospitali ya Kikongo unakamilika lakini hususani upatikanaji wa vifaa tiba na kutoa kipaumbele kibajeti pia katika mashirika yetu ya Mzinga na

Nyumbu ili yaweze kuendelea zaidi, lakini pia mmesisitiza kutekeleza maoni yenu yaliyotolewa katika vipindi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nimeyasema kwa muhtasari lakini tu nipende kuwahakikisha tu kwamba yote tutayazingatia na nitatolea ufafanuzi machache sana.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nianze kwa kusema na kulitaarifu Bunge lako Tukufu na kuanza kusema kwamba tangu Jeshi letu limeanzisha tarehe 1 Septemba, 1964 limeendelea kukuwa na kuimarika na kinyenzo, kizana, kiteknolojia na kiweledi kulingana na mabadiliko yanayoendelea duniani na mahitaji ya wakati na huu ndio msisitizo wenu Waheshimiwa Wabunge na tutaendelea kuuziangatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwa kuzingatia hali hii Jeshi letu limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa weledi na Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba inaliwezesha Jeshi letu ipasavyo. Kiasi cha pesa kilichotelewa nimekielezea, lakini ninashukuru sana Kamati pia imeelezea na kuridhishwa kwamba mtiririko wa pesa umekuwa ukiendelea kulingana na hali ilivyo huu ni mwezi Aprili. Kwa hiyo, hizo asilimia mlizozitaja kati ya 70% na Wizara ikiwa na 42% zitaendelea kufanyiwa kazi na nina imani kufika mwisho wa mwaka wa fedha asilimia hizi zitakuwa zimeongezeka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashirika yetu kwamba yapewe uzito kibajeti na yaweze kutekeleza majukumu yake, nipende kusema tu kwamba hili linafanyika na ninaomba nitoe shukrani sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita ukiangalia mtiririko wa fedha tangu Serikali hii imeingia madarakani umekuwa na mabadiliko makubwa sana. Kumekuwa na ongezeko kubwa sana lakini pia kipaumbele kimetolewa kwa kiasi kikubwa sana katika sekta ya ulinzi na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kwamba rasilimali fedha ni chache, teknolojia inakuwa kwa haraka Serikali imesisitiza kwamba lazima tuingie ubia na sekta binafsi. Kwa hiyo, katika mashirika yetu haya mawili tayari taratibu zinaendelea na kama

nilivyoelezea kuingia ubia na sekta binafsi tutaanza na Nyumbu. Kwa hiyo, kiteknolojia tutapata manufaa zaidi kuliko sisi kujifungua ndani. Kwa hiyo, pesa itatolewa na Serikali, lakini ubia tutakaofanya na sekta binafsi utayaongezea mashirika yetu uwezo zaidi. Kwa hiyo, tunaendelea na hili, lakini haimaanishi kwamba Serikali haitaendelea kutoa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho nipenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tunaelewa umuhimu na tunalifanyia kazi. Ni kuhakikisha kwamba tuna hospitali inayojengwa Msalato inaweza kufanya kazi mara moja itakapokuwa imekamilika. Hiki ni kipaumbele kwa sababu hospitali hii ni hospitali kubwa sana itakuwa ni miongoni wa hospitali kubwa hapa Jijini Dodoma na hospitali hii pamoja na kuwatibu wanajeshi itakuwa inatoa huduma pia kwa wananchi wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua hilo kwa umoja wetu kama Serikali hatufanyi kazi pekee yetu hela inatoka Serikali Wizara ya Fedha wametoa kipaumbele lakini kama mnavyofahamu tumekuwa tukifanya kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani na nipende kuishukuru sana Serikali ya Ujerumani kwa msaada waliotupatia na mpaka sasa hivi tuna hitajio la shilingi 14,779,682,000 kwa ajili ya vifaa tiba na dawa. Tumeshakaa pamoja Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhakikisha kwamba pesa hizi zinapatikana na hata ninaongea hapa tayari vifaa tiba vimeshaanza kutolewa na madhumuni ni kwamba mara tu ujenzi wa majengo unapokamilika vifaa tiba viwe vimekwishaingizwa na hospitali hii ifanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwashukuru sana Kamati mmekuwa mstari wa mbele kupigania hospitali hii. Tunawashukuru sana mmekwisha kwenda kutembelea hospitali hii si chini mara mbili na muda wote mliokwenda mmetoa ushauri na ninafurahi kusikia mnakiri kwamba ushauri wenu tumeuzingatia, tunafanya kazi sana kwa karibu na Wizara ya Afya, Waheshimiwa Mawaziri wamekwisha kwenda Wizara ya Afya kujionea hali ili tuweze kuweka mpango wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ninaomba nikitolee ufafanuzi katika Bunge lako Tukufu ni kuhusu barabara za usalama; hili limeongelewa sana na Waheshimiwa Wabunge limeongelewa sana na Kamati ya Kudumu na niwashukuru pia kwa kuendelea kulisukuma suala hili. Kwa uzito mlioutoa nilikwishakaa na wenzangu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI nilishakaa pamoja na Waziri wa Ardhi, nilishakaa na Waziri wa Fedha na Waziri wa Ujenzi. Tulikaa pamoja tukasema sasa hili suala inabidi tuliwekee mkakati mahususi tuone tunatoka namna gani hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tulichokifanya tumeunda Kamati ya Kitaalamu ambayo itapitia vyanzo vyote vya fedha tulivyonavyo na kuona tunafanyaje ili tuweze kutatua hii changamoto ambayo imekuwa ni changamoto ya muda mrefu. Kamati hii ya kitaasisi inatarajiwa kuwasilisha taarifa yake mwisho wa mwezi huu. Kwa hiyo, nina imani baada ya kupata hii taarifa tutaona tunakwenda namna gani ili tuweze kutatua kero hiii ambayo imekuwepo kwa muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, nipende tu kusema kwamba ninakushukuru sana kwa jinsi ambavyo umeendesha mjadala wa hotuba hii. Ninawashukuru sana Kamati, niwathibitishie kwamba yale yote mliyoyasema, mliyotoa shauri tutayafanyia kazi kwa ukamilifu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. Sasa tunaendelea.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Matumizi.

**SPIKA:** Kamati ya Matumizi.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 38 – Ngome**

Kifungu 1001 - *National Defence Headquarter (NDHQ)*……...........Sh. 2,712,995,141,000
Kifungu 1006 - *Defence Forces Headquarter Command (DFHQC)*….....................Sh. 3,658,377,000
Kifungu 1007- *Land Forces Command (LFC)*….........Sh. 4,644,700,000
Kifungu 1008 - *Air Forces Command (AFC)*…..........Sh. 4,189,108,000
Kifungu 1009 - *Navy Command (NC)*...................….Sh. 2,445,233,000
Kifungu 1010 - *Military Hospitals (MH)*…....................Sh. 4,196,670,000
Kifungu 1011 - *Reserve Force Command (RFC)*…...Sh. 1,599,975,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**

Kifungu 1001- *The National Service Force* …........Sh. 567,023,845,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources*

*Management*....................................Sh. 21,382,742,400
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*……..........Sh. 330,350,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division*…….........Sh. 867,701,000
Kifungu 1004 - *Internal Audit Unit*……..........................Sh. 335,577,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*…......Sh. 274,640,000
Kifungu 1006 - *Legal Services Division* …......................Sh. 375,757,200
Kifungu 1007 - *Government Communication Unit*…..Sh. 220,760,200
Kifungu 1008- *Monitoring and Evaluation Unit*…........Sh. 180,710,800
Kifungu 1009 - *Information and Communication Technology Unit*…..............................Sh. 444,200,000
Kifungu 2001 - *Industries, Construction and Agriculture Division*...................................................Sh. 471,472,000
Kifungu 2002 - *Military Research and Development Division* …........................................Sh. 1,037,139,400
Kifungu 2004 - *Estate Management and Building Consulting Division*…..............................Sh. 441,286,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 38 – Ngome**

Kifungu 1001- *National Defence Headquarter (NDHQ)* …......................Sh. 48,867,636,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 39 – Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)**

Kifungu 1001- *The National Service Force*…..........Sh. 9,929,926,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 57 – Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kifungu 1003- *Policy and Planning Division* …...............................Sh. 0
Kifungu 1008 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh. 350,000,000
Kifungu 1009 - *Information and Communication Technology Unit*…..............................Sh. 3,500,000,000
Kifungu 2001 - *Industries, Construction and Agriculture Division*….........................Sh. 38,040,000,000
Kifungu 2002 - *Military Research and Development Division*…................Sh. 199,254,219,688
Kifungu 2004 – *Estate Management and Building Consulting Division*…........................Sh. 18,855,780,312

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Mtoa Hoja Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari la 2023, Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ninaomba kutoa Taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake, ninaomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono.

Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wote mmeafiki. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya ninyi kuhojiwa na wote kusema ndio, sasa nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Pia, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kupitishiwa bajeti yake na Bunge lakini pia tumtakie kila la heri katika utekelezaji wa yale ambayo yamesemwa huyo. Pia nimpongeze Katibu Mkuu na viongozi wote chini ya Wizara hii ambao wanafanya kazi kwa kushirikiana vizuri kabisa na Kamati yetu, tunashukuru kwamba ushauri unaotolewa na Kamati mmeufanyia kazi lakini pia ule uliotolewa Mheshimiwa Waziri umeahidi kwamba mtaendelea kuufanyia kazi. *(Makofi)*

Pia nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati yetu inafanya kazi nzuri sana tunawashukuru Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti lakini na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kuendelea kufanya kazi vizuri kwa ushirikiano na Wizara hii. Na ninyi pia pamoja na shukurani hizo, tuwashukuru pia Wabunge wote kila mmoja kwa

nafasi yake namna ambavyo anaendelea kushiriki mijadala, lakini pia kutoa mawazo yake juu ya utendaji wa Wizara hii. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, nitangaze wageni ambao waliingia baadaye baada ya tangazo la kwanza kwamba limeshatangazwa.

Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika na tutaanza na wageni wa kwangu; hawa ni viongozi wa Shule Kuu ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; yupo Dkt. Laurean Mussa, huyu ni Amidi wa Shule Kuu ya Sheria, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Dkt. Veronica Buchumi; yupo pia Dkt. Goodluck Kiwory na wameongozana na Ndugu Edward Budeba, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Stergomena Tax ambao hawakupata nafasi ya kutambulishwa awali; yupo Luteni Jenerali (Mstaafu) Wynjones Mathew Kisamba ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Teknolojia la Nyumbu, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Meja Jenerali (Mstaafu) Farah Abdi Mohamedi ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT); na Brigedia Jenerali Bright Livingstone Msuya, huyu ni Kaimu Mkuu wa Mipango na Maendeleo Jeshini, karibuni sana na ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Geofrey Renatus Nyoni, Mdhibiti Mkuu wa Jeshi; Brigedia Jenerali Seif Athuman Hamis, Meneja Mkuu Shirika la Mzinga; yupo pia Brigedia Jenerali Athanasius Kaihura Kamuhabwa, Kaimu Mkurugenzi Mkuu *Tanzania Automotive Technology Centre,* karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo Brigedia Jenerali Petro Elikana Ngata, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Thobias Andengenye, huyu ni Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji (Mstaafu) huyu ni Mkuu wa Mkoa wa Kigoma; karibu sana. *(Makofi)*

Ninaona makofi ya kutoka Kigoma kumbe yanatokea sehemu moja. Haya, ahsante sana. *(Makofi)*

Yupo Kanali Patrick Kenan Sawala, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara; yupo Kanali Evans Alfred Mtambi, Mkuu wa Mkoa wa Mara; Mheshimiwa Daniel Godfrey Chongolo, Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Mheshimiwa Hajat Fatma Abubakari Mwassa, Mkuu wa Mkoa wa Kagera. Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Dio Bamwenda, shemeji wa Mheshimiwa Dkt. Tax, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni wengine wa Mheshimiwa Dkt. Tax ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Makao Makuu ya Jeshi na Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia wapo wanamichezo waliofanya vizuri Jeshini; na pia upo uongozi wa *TUGHE,* wakiongozwa na Mwenyekiti Ndugu Markus Nyanda, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wageni 21 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati ambao ni Kwaya ya Sifuni wa Kanisa la Anglikana kutoka Veyula, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wanafunzi 96 na walimu watatu wa Shule ya Msingi *St. Ann's* kutoka Mbarali, Mkoa wa Mbeya, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia kwa taarifa ambayo tumesomewa hapa kwamba majeshi yetu yapo katika hatua mbalimbali kwenye maeneo mbalimbali ya kuhakikisha mipaka

yetu inakuwa salama, basi nitumie fursa hii kumshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama Amri Jeshi Mkuu. *(Makofi)*

Pia nimshukuru Mkuu wetu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali J. J. Mkunda kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania tunaendelea kuwa salama katika nchi yetu na tunawatakia kila la heri katika kazi hiyo ya kuhakikisha mipaka yetu inakuwa salama. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo basi ninaahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.45 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 21 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*